

# KITENDAWILI



Habari za asubuhi, marafiki. Ni majaliwa kuwepo hapa tena asubuhi hii. Na, sasa, waliniambia walikwisha kuwa na mkutano maalumu, na waliandika taarifa. Na walinitaka mimi kuja kusikiliza taarifa hizo, kuhusu, kama ningekuwa na neno dhidi yake au la, kuhusu, walisema kulikuwa na kitu kuhusu mahojiano, wamekuwa na matatizo. Nafikiri hilo ni zuri sana, namna hiyo. Ninakubali jambo hilo. Hilo linanipa nafasi basi kwamba naweza.

<sup>2</sup> Kuna wengi sana, nadhani kuna kama mia sita kwenye orodha ya wanaongojea, sasa hivi, unaona, kuhusu mahojiano maalum. Nami ninawajibika kimaadili kwa neno langu, kukaa na kila mmoja mpaka kwamba tusikie kutoka kwa Mungu, kumhusu mtu yule, unaona. Na basi kama ukifanya hilo, waweza uwe na mtu mmoja kwenye orodha ya wanaongojea, au pengine ukiwa na mtu yule mmoja, ungojee kwa majuma mawili au matatu kwa ajili ya mtu yule mmoja, unaona, mpaka hasa tusikie kutoka kwa Mungu; tukutane pamoja, tukiomba pamoja; tukirudi, kuachana; kukusanyika pamoja tena, kuomba pamoja, mpaka tupate BWANA ASEMA HIVI kwa ajili ya mtu yule. Vema, katika wakati huo, unaona, kuna mambo mengine.

<sup>3</sup> Sasa kwa njia hii, namna ninavyolielewa, vema, kwamba kila mmoja ataandika mahitaji yake, yo yote yale, na kunipatia tu hayo. Na kuniachia, na kisha kuniacha niombe kwa ajili ya hitaji hili, kisha naweza kuwaita watu hawa mahali ambapo . . . Je, hivyo, hivyo ndivyo ilivyokuwa? [Ndugu Neville anasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, hilo, hilo ni zuri. Unaona, na ndipo labda wakati ninangoja pamoja na mtu huyu mmoja, ningeweza kupata watu mia moja, mia mbili, papo hapo kwa hili moja, kundi hili papa hapa, wakati ambapo ninangojea kwa ajili ya huyu mmoja. Sababu, namna hiyo, itanipa nafasi basi ya kupata kuwaona watu zaidi. Na—napenda hilo hasa. Ye yote aliyepata wazo hilo, vema, naamini ni zuri kweli. Hilo sawa.

<sup>4</sup> Na kwa hiyo, sasa, hili limekuwa kwa namna fulani juma muhimu sana kwangu mimi, haya majuma machache yaliyopita. Nimekuwa kule nje mbele za Bwana wetu, kama mnavyofahamu.

<sup>5</sup> Lakini, ninawaza, kabla ya kuanza ibada, nafikiri mimi . . . Na mmoja ninayemjua, nina mjukuu hapa mahali fulani katika jengo, na pengine . . . Kama yeye ni wa ukoo wa Branham, ana fujo, akikimbiakimbia hapa na pale mahali fulani, labda, kwa hiyo yeye—yeye ndiye apaswaye kusikiliza maagizo haya, kwa hiyo yeye yuko hapa karibu mahali fulani. Nafikiri kuna ibada ya kuwekwa wakfu, na kwa mama wengine ambao wana watoto

wao wachanga. Vema, kama Ndugu Teddy, naamini ndiye, atakuja kwenye piano, nasi tutaimba wimbo wetu tunaoujua sana wa siku nyingi kwa ibada ya kuweka wakfu, kwa watoto wachanga, *Waleteni*.

<sup>6</sup> Sasa, watu wengi, katika makanisa mengi, huwanyunyizia maji watoto wachanga. Nasi tunajaribu kufuata tu mwelekeo wa Biblia, kwa karibu kama nijuavyo jinsi ya kuufuatilia. Naam, hakuna mahali katika Biblia ambapo waliwahi kumnyunyizia mtu mzima, licha ya mtoto mchanga. Na hakuna mahali ambapo Mungu aliamuru kunyunyizia, mtoto mchanga au mtu mzima.

<sup>7</sup> Bali kuna mahali, katika Biblia, ambapo waliwaleta watoto wachanga kwa Yesu, Naye akainua mikono Yake akaiweka juu ya watoto wachanga, akawabariki, akasema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu.” Sasa hiyo ndiyo njia—njia yetu ya kutenda jambo hilo hapa. Na sasa, kama watumishi Wake, tunawachukua tu mbele—mbele za Mungu, katika maombi; na kama kuna ye yote hapa ambaye ana mtoto wake mchanga hajawekwa wakfu.

<sup>8</sup> Hatuamini katika kubatiza, kwa namna yo yote, hao watoto wachanga. Kwa sababu, hawana dhambi. “Wamezaliwa katika dhambi, wakaumbwa katika uovu, wakaja ulimwenguni wakisema uongo,” bali hawana jambo la kutubia. Na ubatizo ni kwa toba na ondoleo la dhambi. Kwa hiyo, mtoto wao mchanga hana jambo la kutubia; na Yesu alipokufa msalabani, Yeye alitakasa dhambi yote. Na sasa tunapokuwa wakubwa vya kutosha kujua kwamba yatupasa kutubu kwa yale tumetenda, basi tunabatizwa, na kutambua kwamba Kristo alitufia. Kitoto hicho kichanga hakiwezi kutambua hilo, kwamba Kristo alikufa kwa ajili yake; bali tunapokuwa wakubwa vya kutosha kutambua kwamba Kristo alitufia, ndipo tuna—tunabatizwa basi katika mauti Yake na kufufuliwa kwa ufufuo Wake. Bwana akipenda, Jumapili ijayo nitazungumzia hilo, Bwana... kama Mungu akipenda.

<sup>9</sup> Naam, kwa hiyo, tunawaleta na kuwaweka wakfu. Mama ye yote, kanisa lo lote, imani yo yote ama rangi yo yote, kitu kingine cho chote, tunawaweka wakfu watoto wadogo wote kwa Bwana Yesu Kristo.

<sup>10</sup> Sasa, Ndugu Teddy, kama utatuongoza kuimba huu, *Waleteni*, tafadhali. Vema, hebu sote pamoja sasa.

Waleteni, waleteni

Waleteni toka kwenye maeneo ya dhambi;

Waleteni, waleteni,

Waleteni watangao kwa Yesu.

<sup>11</sup> Kwenye ono nililoona, baada tu ya kufariki kwa mama yangu, huo ndio niliokuwa nikiongoza, huo wimbo, ni *Waleteni*, wakati watoto wadogo, wangewaleta.

Tafadhali njoo, Ndugu Neville.

<sup>12</sup> Namjua mvulana huyu. Billy anasema, “Usimwangushe. Usimwangushe.” Ndiyo. Huyu ni William Branham, tupo watatu wamesimama hapa pamoja, akina William Branham, vizazi vitatu na majina matatu. Ananiangalia mimi asubuhi hii, pia. Kuna Kitu fulani kuhusu wao, kwamba kwa namna fulani huonekana wasio na hatia, mnajua. Na jina lake ni William Paul, Junior. Na kwa hiyo tunashukurani, nashukuru asubuhi hii, kumpa Bwana Yesu, toka kwenye mikono ya baba yake (mwanangu), huyu mjukuu, kwa maisha ya utumishi; baraka juu ya baba na mama.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>13</sup> Baba yetu wa Mbinguni, Mwenye Neema, najua ninasonga mbele barabarani, ninapomshikilia mjukuu wangu mkononi mwangu.

<sup>14</sup> Bali namfikiria Yakobo, alipowaleta wajukuu wake katikati ya magoti yake, alipokuwa mzee, Efraimu na Manase; aliwabariki watoto hao, na akawapa baraka za rohani ambazo zimedumu hata siku hii. Jinsi alivyopishanisha mikono yake toka mmoja, hadi mwingine, akichukua baraka toka kwa Wayahudi akawapa Mataifa, katika msalaba. Mungu wa Mbinguni na akaribie sasa.

<sup>15</sup> Huyu mjukuu ambaye Wewe umenipa mimi, Bwana, kupitia mwanangu na mkwe wangu! Ninamfikiria yeye alipokuwa tasa, asingeweza kuzaa watoto, nasi tulipokuwa tunashuka siku ile kutoka Yakima, Washington, alipokuwa analia, akasema, “Laiti ningepata mtoto.”

<sup>16</sup> Roho Wako akaja kwenye gari, na hapo nikasema, “Utampata.” Na leo ninamshikilia huyu mvulana mdogo mzuri mikononi mwangu; Neno Lako lililonenwa, ahadi Yako.

<sup>17</sup> Sasa, Bwana, katika urahisi wa matendo yetu, twamuweka mtoto huyu, kwa imani, katika mikono ya Bwana Yesu; kwamba Yeye, akiwa yupo hapa katika hali ya Roho Mtakatifu, atamchukua mtoto huyu katika mikono Yake na uangalizi Wake, na atamwongoza maishani. Mpe afya na nguvu, maisha marefu, kama Wewe ukikawia. Mtoto huyu na atumike kwa utukufu Wako. Nguvu ya Mungu aliye hai na ikae juu ya mtoto huyu. Kama akiishi kuwa mwanamume, na Yesu akawie, jalia kwamba aihubiri Injili. Nguvu za Mungu ambazo zilimkabidhi kwa mama na baba yake, jalia Hizo zisimwache kamwe.

<sup>18</sup> Mbariki baba yake na mama yake. Jalia wakuzwe, na yeye amkuze mtoto huyu katika hali ya Kikristo. Kwamba, mafundisho yote yanayowezekana ya kibinadamu ambayo wanaweza kumpa, mtoto huyu atayapata.

<sup>19</sup> Sasa, Billy Paul Branham, Junior, ninakutoa kwa Mungu Mwenyezi, katika kuwekwa wakfu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

20 Kuna jambo fulani kuhusu watoto wachanga, yaani, ninalifikiria ni la kupendeza sana!

21 Namkumbuka Loyce, yeye alilia na akashikilia mikono yake. Ni mwenye wasiwasi kwelikweli. Loyce ametoka kwenye dhiki kuu, ni msichana mdogo wa Kentucky ambaye hasa amekuwa na maisha magumu. Na yeye... Usiku mmoja, Yesu alimtokea, akiwa amesimama kwenye baridi. Naye akaja, akikimbilia nyumbani, yapata usiku wa manane, yeye na Billy, baada ya kuoana. Nao... chini kwenye kitanda cha watu wawili cha kukunja kule, nikamkumbatia na kumwongoza kwa Bwana Yesu.

22 Alitaka watoto mno. Walikuwa wameoana miaka kadha. Basi tulipokuwa tukishuka kutoka Yakima siku moja, alikuwa kwa namna fulani akilia. Ilikuwa ni... Roho Mtakatifu alikuja na kumwambia tatizo lake la kike ambalo alikuwa nalo, alitaja sababu hakuweza kuwa na watoto. Halafu Roho Mtakatifu akaja tena, na akalaani tatizo lile la kike na kumpa ile baraka. Nimemweka wakfu sasa hivi. Kuna...

23 Ninayo baadhi ya mambo madogo yaliyoandikwa hapa, ambayo nataka kunena kwanza, kabla ya kusoma fungu la maneno. Kwanza, ni mikutano ya siku za usoni, nimeandika. Hiyo ni Jumapili ijayo, Bwana akipenda. Najua barafu inaanguka na kuna hali mbaya barabarani.

24 Na tunao watu hapa toka Georgia, na Alabama, na Florida, na Ohio, na Illinois. Na—na kundi hili dogo la watu limeundwa kutoka kila mahali.

25 Baadhi ya watu wananiambia, kasema, “Nilipitia kanisani mwako chini huko, Billy, asubuhi kule. Kuna leseni toka kila mahali nchini humu.”

Nasema, “Ndiyo.”

26 Mmoja *hapa* na mmoja *pale*, hivyo ndivyo ninavyofikiria Bibi-arusi atakuwa. “Wawili shambani; Nami nitachukua mmoja, niache mmoja,” kadhalika.

Na si—sipendi watu waendeshe gari kwenye barabara zenye barafu.

27 Na mimi nikijua, pia, kwamba mara baada ya Krismasi sasa, nita—nitaondoka, niende kazini, Bwana akipenda. Nina yapata ibada kumi na tano mbalimbali zilizopangwa sasa.

28 Nami nataka kutangaza, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, nataka kufundisha juu ya Ujumbe ambao ni muhimu sana, kwangu. Nimekuwa nikijifunza, juma hili na juma lililotangulia, juu ya historia ya Biblia. Nami nataka kuzungumza juu ya somo la *Ukristo Dhidi ya Upagani*, kwa hiyo, au, *Ibada ya Sanamu*; Jumapili ijayo.

29 Na basi Jumapili ijayo ni siku ya Kuamkia Krismasi, Jumapili ijayo; na Jumapili, juma moja, ninamaanisha,

samahani. Jumapili, juma moja, ni siku ya Kuamkia Krismasi. Sasa kama nikitoa Ujumbe, na wale, baadhi ya rafiki wapenzi wanatoka Alabama na Mississippi na Georgia, na kila mahali jinsi hiyo, watoto wadogo hakika watahuzunika kwenye usiku wa Krismasi. Na kama Bwana akiliweka moyoni mwangu kuliletea kanisa Ujumbe wa Krismasi, nitauleta basi, Mungu akipenda, namwahidi kila mtu anayetoka nje ya mji, unaona, nitawapelekeeni ukanda huo mimi mwenyewe, unaona. Kwa hiyo haitawalazimu kuwaacha watoto wenu usiku wa Krismasi, usiku wa Kuamkia Krismasi. Na ndipo nita—nitawapelekeeni ukanda huo, kwa shukurani zangu za mkutano. Basi kumbukeni tu hilo.

<sup>30</sup> Jambo jingine, mwajua, ninyi—huwezi kumtazamia kila mtu kuamini kila kitu usemacho. Hali—haiwi namna hiyo.

<sup>31</sup> Nilisahau asubuhi hii, nikikimbia haraka, kusudi nifike hapa. Ikatukia mimi kuangalia juu...Ndugu Woods alimleta mke wangu na hao wengine huku. Ni—nikaangalia juu, na ilikuwa karibu wakati wa kuanza ibada humu, wa kuja kwangu. Nao waliniambia, Billy aliniita usiku uliopita, naye akasema walinihitaji mimi hapa asubuhi hii, kusikiliza taarifa hizi zikisomwa toka kwenye mkutano wa mwisho.

<sup>32</sup> Nilikuwa naenda kuleta historia, kujaribu tu kunyoosha jambo fulani nililosema. Haidhuru unajaribu kulifanya wazi jinsi gani, bado kuna mtu fulani asiyelielewa. Ni kuhusu madhabahu kanisani. Unaona? Mtu fulani alisema, “Ndugu Branham haamini kuweka madhabahu kanisani.” Ninaamini katika kuwepo kwa madhabahu kanisani. Unaona? Bali madhabahu hazikuwa mahali ambapo watu huja kuomba. Hapajawa kamwe na wito wa madhabahuni katika wakati wote kwenye Biblia. Hakuna kitu kama hicho.

<sup>33</sup> Nami nataka kuwaleteeni, nitawaletea Jumapili ijayo, katika historia ya kanisa la mwanzoni, kwamba sababu ya kutokuwa na madhabahu kanisani. Ni kwa sababu, kusujudu madhabahuni ni ibada za upagani, na si wazo la Kikristo hata kidogo. Naam, nitazungumzia juu ya hilo, pia, Jumapili ijayo. Lakini hakukuwa na madhabahu katika kanisa la mwanzoni, kufanya mwito wa madhabahuni. Hapakuwa na cho chote isipokuwa chumba kitupu. Basi. Hakuna sanamu ya kusulubiwa, hakuna cho chote, hamna cho chote chumbani isipokuwa sakafu tupu. Watu hao walikuwa Ka—Kanisa la kipentekoste katika siku za mwanzoni, kama nitakavyowaletea toka kwa wanahistoria mbalimbali, Jumapili ijayo, Bwana akipenda. Nami nataka kuwaleteeni hilo toka kitabu cha Ironside kiitwacho *Kanisa la Mwanzoni la Wasafiri*, na kutoka *Babiloni Mbili* cha Hislop, kutoka *Wazee Waliotangulia Nikea*, *Baraza la Nikea*, loo, vingi mno, maandiko ya Hazeltine ya kanisa la mwanzoni, na vingine mbalimbali, unaona. Kukuonyesha kwamba hakuna mahali po pote...

<sup>34</sup> Hata huko Ireland, ambako nimezuru katika kanisa ambako Wakatoliki wanamwita mtakatifu wa Kikatoliki, Mtakatifu Patrick, lakini hapakuwa katu katu na kipengele cha historia mahali po pote ambacho kinasema hilo. Kwamba Mtakatifu Patrick hakuwa kingine ila mpinzani wa kanisa la Kirumi. Hakuna mahali po pote. Hapana mtu awezaye kutoa historia yo yote ambayo itaonyesha jambo hilo, kwamba yeye alikuwa Mkatoliki. Yeye, ninino zake, shule zake zote zilikuwa huko Ireland ya kaskazini. Basi wakati huyu mfalme wa Kikatoliki alipotawazwa Uingereza, aliwa kumi elfu ya wafuasi wa Mtakatifu Patrick. Na kanisa hilo bado linasimama kule leo hii, shule zake, zote huko Uingereza ya Kaskazini.

<sup>35</sup> Na hapo unapowasikia wakisema, “Mtakatifu Patrick alifukuza nyoka wote kutoka Ireland,” mwajua ilikuwa ni nini, ukweli wake wa kihistoria? Aliamini katika pentekoste, kwamba ana Nguvu za kushika nyoka, kukamata nyoka. Na hiyo ndiyo sababu hayo yanasemwa, yalivyoanza.

<sup>36</sup> Pia kusulubiwa kwa Petro, kichwa chini, huko Rumi, hakuko katika kitabu cha wafia imani. Nami nimechunguza kila kimoja, kila mahali, na nimesoma wanahistoria, kila kitu ninachojua, na hakuna hata Andiko moja ambalo lilisema ama Paulo au Petro aliuawa huko Rumi. Ni mafundisho ya sharti. Lilianzishwa na kanisa la kwanza la Kirumi, na si Kweli, unaona. Kuna mambo mengi. Nitafikia hilo Jumapili ijayo.

<sup>37</sup> Kisha jambo jingine ninalosikia habari zake sana. Mtu fulani aliniambia, mhubiri anayejulikana sana, yeye alisema, “Ndugu Branham, kwa nini usiwaache hao wanawake?” Alisema, “Unajua, watu wanakuchukulia wewe kama nabii. Kwa nini usiwafundishe mambo ya juu ya kiroho?” Huenda ikawa mtu huyo ameketi hapa sasa. Kama ndivyo, nataka uelewe hili, ndugu. “Kwa nini usiwafundishe mambo ya juu ya kiroho, ambako unapanda, na kuwaacha wao wapande huko; badala ya kuwaambia wao kuhusu kutokata nywele zao, na mavazi wanayopaswa kuvaa?”

<sup>38</sup> Kama upo hapa, au unasikiliza kanda, ndugu. Kama siwezi kuwatoa katika shule ya watoto wadogo, nitawafundishaje aljebra? Hawana heshima na uadilifu wenyewe maishani mwao, hata kuruhusu nywele zao zikue, na kuvaa mavazi kama mabibi, utawafundishaje mambo ya kiroho? Unaona? Wawezaje. Hawajui la kwanza, hawajui ABC. Na kujaribu kuwafundisha jambo fulani la juu, kuwapa elimu ya chuoni, huku hawajui ABC? Acha wajifunze ABC kwanza, halafu tuta—tutaifikia hiyo.

<sup>39</sup> Sasa, juma lililopita mlikuwa na m—mtu maarufu hapa kwenye mimbara, kuchukua mahali pang'u. Huyu alikuwa Ndugu William Booth Clibborn, ambaye anajulikana, miongoni mwa wahubiri wote, kuwa kiongozi wa wahubiri; mtu maarufu, mhubiri maarufu, maarufu sana. Kwa kweli, ni mmoja wa walio

wazuri kuliko wote nchini, mahali po pote. Mtu huyo anaweza kuihubiri Injili katika lugha saba mbalimbali, kwa hiyo unaweza kuwazia alivyo yeye. Na yeye ni mhubiri wa Injili yote.

<sup>40</sup> Yeye ndiye aliyekuwa upande wangu katika mjadala ule, wa hao wahubiri saba wa Church of Christ wakati ule. Na kama kuliwahi kuwa na watu niliowasikitikia, ni hao watu baada ya yeye kumaliza kujadiliana nao. Si—sijawahi kusikia mambo kama hayo maishani mwangu. Hata walisimama wakaanza kwenda zao. Akakutana nao mlangoni, akasema, “Nalifikiri mlitaka kuzungumzia juu ya kuponywa Kiungu?”

<sup>41</sup> Naye ni mtu wazi sana, hata hivyo, ni wazi sana. Aliwaita tu cho chote alichoweza, hata “majuha” na kila kitu, unajua. Kwa hiyo, yeye, yeye ni wazi kabisa, na hivyo ndivyo alivyo tu. Kama angeukoleza ujuzi ule kwa upendo, ingekuwa kitu kingine, unaona. Na hu—huenda yeye yuko hapa. Ndiyo, bali ni—ninamaanisha hilo, mnajua, hivyo, kama yeye angekuwa mzuri katika jambo hilo. Bali, loo, jamani, yeye ni Mwingereza, naye anaweza tu kuchochewa hasa.

<sup>42</sup> Lakini aliwakabili mlangoni, na akawanyoshea kidole chake usoni mwao, kasema, “Hebu muthubutu kumrukia tena,” yaani mimi, akasema “nitawaweka wazi hadharani, nami kweli nitawafanya kundi la punda kwelikweli,” akasema. Nami sijawasikia kamwe tangu hapo, unaona. Ndiyo. Siwalaumu. Singemkaribia, pia. En-hee. Ndiyo, kwa sababu hutapata kamwe neno la kuepa, kwa Ndugu Booth.

<sup>43</sup> Mhubiri wa ajabu, mtu mzuri, Mkristo mzuri, msafi, mtu mwadilifu, kadiri nijuavyo lo lote kumhusu yeye, na nimemjua kwa miaka kadha. Nilipata kusikiliza kanda yake, yale aliyowahubiria ninyi, kuhusu jinsi Mungu alivyokuwa mtakatifu na alivyo juu, na jinsi ambavyo tulizaliwa katika dhambi; na kitu gani mtu angeweza kufanya ambacho kingeleta, angeweza kumwambia Mungu la kutenda. Unaona? Na hayo kweli yalikuwa mazuri sana.

<sup>44</sup> Naam, sababu ya kuondoka kwangu wakati huu, nilikuwa na juma la kufunga pamoja na maombi, ambalo liliniongoza kupata uamuzi.

<sup>45</sup> Na nina swichi ndogo hapa, inapaswa kuwepo mahali fulani, ambayo hukatiza, hukatiza jambo ambalo sikutaka. Loo, basi. Ndiyo hii. Ninalotaka kwenye kanda, na usichotaka kwenye kanda. Kwa hiyo, ndugu zanguni, kama kanda yako imevurugika kidogo, vema, usi. . . Unaweza kukata sehemu hiyo. Sasa, lakini mle ndani, namna hiyo, wengi sana wakinasa, wakati Ndugu Mercier na hao wengine ndio tu wangenasa kanda, mbona, ningewataka wakate sehemu isiyotakiwa kwenye kanda nje huko kabla ya kuziruhusu zisambazwe. Bali katika huu, mtu ye yote anaweza kuzinasa sasa, unaona, ye yote anayetaka kuzinasa anaweza kuzinasa. Na kwa hivyo ya—

yanibidi kuzikatiza sehemu zisizotakiwa mimi mwenyewe, toka kwenye swichi hii papa hapa, nisilotaka kusema, kuliacha liende kwenye kanda.

<sup>46</sup> Sababu, yapo baadhi ya mambo niwezayo kuwaambia ninyi nyote hapa, ambayo hakika nisingetaka kuyatoa kwa watu. Sababu, waacheneni. Iwapo kipofu atamwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili, kwa vyo vyote, unaona. Kwa hivyo, hebu usiwakwaze. Kama Yesu alivyosema, “Usiwakwaze hao Mafarisayo.” Kasema, “Kama wanataka kiasi fulani, kama wanataka fedha ya ushuru, shuka uende ukatupe ndoana baharini; ukatwae samaki wa kwanza, ukatoe shekeli mdomoni mwake, uende ukawalipe.” Kasema, “Msifanye hivyo, msiwakwaze, waacheneni.”

<sup>47</sup> Bali katika maisha yangu yote, tangu nimekuwa mvulana mdogo, nime. . . Bwana amenipa maono sikuzote, jambo ambalo tunalijua vyema hapa kanisani na, nina hakika, katika nchi ambako kanda hizi zitasafiri pia, kuhusu maono. Na huku Biblia hii imefunguliwa mbele zangu, na Mungu Ambaye mbele Zake ninasimama, sijajua kuhusu moja ya hayo likishindwa. Yamekuwa sikuzote sawa kabisa.

<sup>48</sup> Nami nilikuwa na ono majuma machache yaliyopita, kama majuma matatu sasa Jumanne hii inayokuja; ambalo lilinipeleka magotini, na nje huko nyikani, kufunga na kuomba. Nami nilivaa (kwa kuwa ni baridi) nguo nzito za ndani, kusudi nizitumie kwenye safari za kuwinda, nisije nikaona baridi sana, huko kwenye pango langu na msituni. Nami nikapanda nikaenda, siyo. . .

<sup>49</sup> Mtu fulani alisema, “Vema, Ndugu Branham, ulipanda kwenda kutafuta? Ilikubidi kupanda kwenda kutafuta ono kwa Bwana.”

<sup>50</sup> Nikasema, “La, huendi. . . Hilitendi jinsi hiyo. Huwezi kuvuta ukatoa cho chote kwa Mungu.”

<sup>51</sup> Mnaona, hiyo ndiyo sababu watu huendelea kusema, kwenye mahojiano, wakisema, “Muombe Bwana. Kaa tu nalo! Kaa tu nalo.”

<sup>52</sup> Nilikuwa na neno la Bwana kumpelekea Ndugu Neville, kuhusu kutabiri juu ya kila mtu ambaye huja madhabahuni hapa. Mungu alimwambia, kwa kweli alimkemea kuhusu jambo hilo, unaona. Msifanye hivyo, mtamshurutisha kimwili ndiposa mtapata nabii wa uwongo. Unaona? Unaona, mwache afanye tu kama vile Roho anavyomwongoza kutenda. Unaona?

<sup>53</sup> Basi, usijaribu kuchomoa cho chote kwa Mungu, sababu huwezi kufanya hilo. Yeye atanena tu. . . Kama vile Balaamu, nabii wa kukodiwa alivyosema, “Naweza tu kunena ambacho Mungu ataweka kinywani mwangu. La sivyo, siwezi kulinena.”

<sup>54</sup> Na ni jambo lilo hilo, napenda utaratibu huu walio nao sasa, hivi kwamba naweza kutafuta ambalo, ambalo tu Bwana angetaka nitende. Hilo ni zuri mno.

<sup>55</sup> Lakini Yesu alienda nyikani, kufunga, baada ya Roho Mtakatifu kuja juu Yake. “Yohana alishuhudia, alipomwona Roho wa Mungu akija juu Yake.” Naye alikuwa amejazwa na Uwezo wa Mungu, Mungu ndani Yake, kisha akaenda Zake jangwani kufunga, baadaye. Si hapo kabla, Roho Mtakatifu apate kuja juu Yake, bali Yeye alienda Zake akafunga baada ya Roho Mtakatifu kuja juu Yake. Unaona?

<sup>56</sup> Na sasa, katika lile ono, huenda nikasema hili. Nililitaja wakati mmoja. Nilikuwa nilikate niliondoe kwenye ukanda, bali naamini nitaliacha tu likae. Mimi. . .

<sup>57</sup> Ilikuwa yapata saa tisa usiku, nafikiri. Nilikuwa nimekwisha amka, nami nikaangalia ambapo mbele yangu, nami nilikuwa ninashuka kwenda Yordani. Ilionekana kana kwamba nilikuwa nimesimama kwenye ramani ya Palestina, na nilikuwa nikishuka kwenda Yordani. Na ilielekea kama niliweza kusikia ule wimbo, “Ninashuka kwenda Yordani,” mtu fulani alikuwa akiuimba. Nami nilipoukaribia huo mto nilitazama nyuma nikaona njia niliyopitia, na nilikuwa nimefikia theluthi mbili ya njia pale, kuelekea Yordani. Basi nikaangalia upande wa pili wa Yordani, nikasema, “Loo, Mungu asifiwe, huko ng’ambo ya pili tu ndiko ambako kuna ahadi zote! Kila ahadi iko katika Nchi ya ahadi.”

<sup>58</sup> Na basi nikapata jirudia, nikawaza, “Hivi ingewezekana pengine nime...ingewezekana kwamba nilikuwa ninaota, maana ni wakati wa usiku?” Unaona, ono ni jambo ambalo unaona macho wazi, kama tu ndoto, unaliangalia moja kwa moja. Na una—una habari kwamba unasimama mahali kama hapa kwenye jukwaa, na ume—umesimama hapa, lakini hata hivyo inaonekana kana kwamba uko kwenye ndoto. Huwezi kulielezea, hakuna njia ya kufanya jambo hilo. Unaona, ni kazi za Mungu. Na njia za Mungu hazielezeki, yabidi zikubaliwe kwa imani.

<sup>59</sup> Kisha nilipokuwa nimeketi pale kidogo, kando ya kiti hiki, ndipo, kwa ghafla, hili hapa likaja tena. Basi nilijua hapo kwamba lilikuwa ono. Basi nilipolipata hilo ono tena, ilielekea kwamba nilikuwa nimeinuliwa juu na kuketi kwenye nji—njia kuu, njia kuu nyembamba, pamoja na ndugu fulani. Sikujua kamwe yule ndugu alikuwa ni nani. Nikaangalia kila upande, nikasema, “Sasa nina hakika na najua hili ni ono, Bwana Mungu yupo hapa.” Na ilielekea kama kila mtu alikuwa na hofu. Nikasema, “Hivi kila mtu anahofia nini?”

<sup>60</sup> Na sauti ikaja ikasema, “Kuna hatari kubwa sana siku hizi. Kuna kitu kibaya sana ambacho ni mauti hapo kinapokupata.”

<sup>61</sup> Nami nikasikia majani yakichakacha, nami nikaangalia, hili hapa linakuja joka kubwa la kutisha likitambaa kwenye majani. Nikawaza, “Sasa, kwa vile ninajua hili ni ono, basi nitaona ni nani huyu—huyu hayawani au mnyama huyu ni nani.” Naye akatambaa juu kwenye barabara kuu. Na mara nilipomwona, nilijua alikuwa Mamba. Sasa, Mamba ni nyoka wa Afrika, ambaye umo lake lina sumu kali sana kuliko wengine wote. Hakuna kilicho na sumu kama Mamba. Na yule nyoka, bila shaka, anawakilisha dhambi, mauti. Unaona? Na kuna. . . Tuna nchini humu, Nyoka Anayetatarika, na Kichwashaba, na Kinywapamba, Nyokakiatu, wengi wa nyoka hao, hivi kwamba, kama huna afya nzuri na mmoja akuume, labda angekuua, lakini kama hukupata msaada wa namna fulani mara moja.

<sup>62</sup> Na basi—basi tunakwenda huko Afrika na India, na tunakuta Swila. Kuna Swila Mweusi, ni nyoka mbaya, akikuuma ni mauti, pia. Na kuna Swila Manjano, ambaye anamzidi yeye sana. Na Swila Manjano, mgonjwa hufa kifo cha kutisha sana, hufa kwa kukosa pumzi. Ana—anapoozesha viungo vya kuvutia pumzi. Na—nao hawawezi kupumua, wao hufungua tu vinywa vyao na kutweta, na kujaribu kupumua, na kufa hivyo. Na nyoka wa aina hiyo ndiye aliyekuwa hatua moja tu kutoka kwa Billy Paul, tulipomuua yule nyoka, huko Afrika.

<sup>63</sup> Halafu—halafu anayefuata ni Mamba, yeye ni mauti. Wakati tu yeye. . . Huyu ana mbio sana hata huwezi kumwona. Hupitia juu ya majani na kujiendesha kwa sehemu ya nyuma ya mkia wake. Huyoo, ndipo amekwenda! Anakuuma usoni, kwa kawaida. Husimama juu sana, akadonoa kwa nguvu sana. Na, anapokuuma, anavuta pumzi mara chache tu na umekwisha. Inakuwa hasa. . . Hapoozeshi tu, huingia kwenye mzunguko wa damu, inashika neva, kila kitu, unakufa tu katika sekunde chache. Hao vijana wenyeji na wavulana wanaoongoza njia, waweza kusema “Mamba,” na watagonganisha vichwa vyao pamoja, wapige yowe, sababu ni—ni kifo tu kwenye sekunde chache, unaona, wakati mmoja anapokuuma.

<sup>64</sup> Na huyu hapo, kwenye njia kuu. Nikawaza, “Haya, basi.” Kwa hiyo nikamwanguka. Naye aliniangalia kwa hasira, akatoa ulimi wake, ndipo huyu hapa anakuja. Bali alipofika karibu sana nami. . . Angekimbia mbio, kisha angeenda pole pole, akatetemeka na kusimama, ndipo kitu fulani kingemzuia. Hangeweza kuniuma. Na angegeuka upande mwingine, na kujaribu kukaribia kutoka upande huu. Naye angerudi na kuanza, akanichakachia akinijia mbio, kisha akaja pole pole, halafu akasimama, ndiposa angetetema hivyo na kusogea nyuma. Hangeweza kunidonoa.

<sup>65</sup> Kisha aligeuka na kumwanguka rafiki yangu, na huyoo akamfukuza rafiki yangu. Nami nikamwona rafiki yangu akiruka tu juu hewani, na juu yake na juu yake na juu yake, akijaribu, na dude lile lilikuwa linamdonoa. Nikawaza, “Loo,

iwapo litawahi kumuuma, itakuwa kifo cha ghafla. Si ajabu kila mtu ametiwa hofu, sababu dude hili linapokuuma ni kifo cha ghafla.” Na—naye alikuwa tu akimdonoa namna hiyo, nami nikatupa mikono yangu juu, nikasema, “Ee Mungu, mrehemu ndugu yangu!” Nikasema, “Kama nyoka yule akimuuma, atamuua.”

<sup>66</sup> Wakati uo huo yule nyoka alinigeukia niliposema hilo, akaniangalia tena. Na Sauti ikaja toka juu yangu, ikasema, “Umepewa nguvu za kumfunga, aliye mbaya sana, au ye yote yule.”

Nami nikasema, “Vema, Mungu, nifanye nini?”

<sup>67</sup> Akasema, “Kuna jambo moja likupasalo kutenda, yakubidi uwe mwaminifu zaidi. Unaona, yakubidi uwe mwaminifu zaidi.”

<sup>68</sup> Nikasema, “Vema, Mungu, nisamehe kwa kutokuwa mwaminifu, na unijalie niwe mwaminifu.” Basi nilipoinua mikono yangu Kwake tena, kulikuwa na Kitu fulani kikuu kilichokuja juu yangu, kikaniinua tu juu, ilionekana kana kwamba mwili wangu wote umejazwa nguvu kwa Kitu fulani.

<sup>69</sup> Nami nikamwangalia yule nyoka. Ndipo akaanza kunijia, na hakuweza kulitenda hilo; bado. Basi nikasema, “Shetani, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninakufunga.” Ndipo yule nyoka, moshi wa samawati ukaruka toka kwake, kisha akajifingirisha na kufanya ile alama kama S, S kubwa ikiandikwa kinyume, alama ya *na*, &. Na inamaanisha “mfunge huyu au cho chote chini yake,” sababu alikuwa ndiye mbaya kuliko wote. Moshi wa samawati ukamtoka, na akajikaba kichwani kwa mkia wake mpaka akafa, alipofanya hii S ya kinyume, alama ile ya *na*, & (kama kiungo, unaona), ukamkaba akafa. Na yule ndugu akawa huru.

<sup>70</sup> Basi nikaenda na kumpondaponda. Nikasema, “Sasa yanibidi nitafute kuhusu jambo hili, kwa sababu ni ono.” Nami nikaligonga lile—lile dude, nalo likageuka hivyo, lilionekana kama mpini, mpini wa glasi kwenye gudulia, na kuifanya tu ngumu kama jiwe la kioo. Nami nikasema, “Wazia hilo, haraka jinsi gani! Ule moshi wa samawati ulikuwa uhai. Na kila kitu kimentoka, kila chembe, na amegeuka akawa kioo.”

<sup>71</sup> Mara Sauti ikaja tena, ikasema, “Unaweza kumfungua, pia.”

<sup>72</sup> Kwa hiyo nikasema, “Basi, Shetani, ili nipate kujua, ninakufungua.” Na lilipotendeka, alianza kuwa hai tena, akifurukuta. Kisha nikasema, “Nakufunga tena, katika Jina la Yesu Kristo.” Na lilipotendeka, ule moshi ukafoka ukatoka kwake tena, naye akajikaba mwenyewe tena akageuka tena kuwa jiwe la kioo.

<sup>73</sup> Basi alipofanya hilo, ile Sauti ikasema, “Sasa yakubidi uwe mwaminifu zaidi kuliko ulivyo sasa, upate kufanya hili.” Ndipo likaniacha, nami nilikuwa nimesimama mle chumbani.

<sup>74</sup> Muda kidogo, nikasikia saa ikipiga kengele, na mke wangu ame. . . akiamka. Watoto, unajua jinsi ilivyo, nadhani, nyumbani kwako, mmoja, “Nitavaa nini leo, mama? Vikoa wapi, viko wapi vitabu vyangu? Na nilifanya nini?” Unajua. Wewe, kama nyumba yo yote, huwezi kujisikia mwenyewe unafikiri, ni vigumu, huku wote wakijaribu kuwa tayari wakati mmoja.

<sup>75</sup> Na—na kwa hiyo nilichomoka kwenda kwenye chumba cha faragha, nami nikapiga magoti, nikasema, “Bwana Yesu, siyajui mambo haya. Basi nifanye nini? Na watoto watakuwa wananiita niwapeleke shule punde kidogo. Nifanye nini?” Nikaangalia huku na huko, na Biblia yangu ilikuwa pale, nikasema, “Bwana, kama Wewe utanisamehe. . .” Siamini katika kufungua tu Maandiko, na kuchukua kitu kutoka katika Biblia na kusema hilo, lakini, kuna nyakati ambazo Mungu anaweza kukufariji kwa kitu kama hicho. Nami nikasema, “Bwana, katika jambo hili la dharura sasa hivi, kabla ya Roho Wako kuniondoka. Nami si—sijui la kufanya. Watoto wana saa moja bado, kabla hawajaondoka. Waweza kunionyesha tafadhali? Kama hilo lilikuwa jambo Wewe unalojaribu kunifahamisha, Baba wa Mbinguni, basi nijalie kulijua.”

<sup>76</sup> Basi nikachukua Biblia hii na kuifungua tu namna *hiyo*, na kidole changu cha gumba kilikaa kwenye I Wakorintho, sura ya 5, aya ya 8, wakati jambo fulani linasema kitu kama hiki. “Unapokuja. . .” Nilikuwa ninapanga kufunga, kwa Bwana. Nilimwambia Yeye ningetoka niende nikafunge. Kasema, “Unapokuja kwenye karamu hii. . .” Ambapo, mfungo katika mwili ni karamu pamoja na Bwana. Tunajua hilo. “Kwa hiyo unapokuja kwenye karamu hii, usije kwa chachu ya kale au chachu ya uovu, na kadhalika; bali uje kwa mkate usiotiwa chachu wa weupe wa moyo na ukweli,” sawa tu na ambalo Yeye aliniambia katika ono lile. “Njoo. . .” Mungu ndiye Hakimku wangu mkuu. “Njoo kwa mkate usiotiwa chachu wa weupe wa moyo na ukweli, hilo ni Neno.” Basi nikaona alilomaanisha Yeye. Kwa kuwa Yeye. . .

<sup>77</sup> Miaka mingi iliyopita, nilipoona Biblia ikishuka, nililiandika papa hapa, ikishuka; na mkono ukashuka toka Mbinguni na ukakielekeza kidole katika Yoshua, na kusoma aya tisa za mwanzoni, na kukoma hapo. Huyu ni Yoshua, alipofika nyikani, bali kamwe hakufanya. . . alikuwa tayari ku. . . Alipokaribia Yordani, Mungu alimwita, kasema, “Leo hii nitaanza kukutukuza mbele ya watu.” Kisha akawavusha wana wa Israeli Yordani, hadi nchi ambayo. . . akawapa, akawagawia, nchi ya ahadi.

<sup>78</sup> Nikaenda mwituni, na nikaomba na kuomba, na kufunga. Na, sasa, nikarudi kwenye mti ule ambako niliwakuta, walipokuwa wale kindi, ambao mlisikia katika Jumbe zingine, unaona, walipokuwa wale kindi. Na nikiwa nimesimama pale, kwenye kama saa tisa au kumi usiku, baada ya kutembea kwa kusitasita msituni na nuru niliyoweza kuona nayo, ili kuufikia ule mti, nikija mapema kwa sababu niliongozwa pale. Ndipo nikakutana Naye. Mungu, nisaidie kudumu kwa uaminifu daima.

<sup>79</sup> Nitasoma kifungu changu sasa. Nimechukua kama kifungu asubuhi hii, kimeandikwa hapa mahali fulani (loo, hiki hapa), Yoshua, katika Kitabu cha Yoshua, sura ya 10. Kweni ninyi mtakaosoma nyuma yangu, au, sura ya 10 na aya ya 12. Na nina saa moja tu.

<sup>80</sup> Na basi nafikiri, sina uhakika, bali ninaamini Billy alisema ametoa kadi za maombi asubuhi hii, kasema, “Hapakuwa na wengi sana, bali baadhi ya watu walitaka kuombewa.” Na mtu ye yote aliye na kadi za maombi, inua mkono wako sasa. Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo. Vema, naam, hilo ni zuri. Sawa.

Sasa aya ya 12 ya sura ya 10 ya Yoshua.

<sup>81</sup> Basi kumbukeni, sasa, wakati ujao, Jumapili ijayo nataka kuzungumza juu ya *Ukristo Dhidi ya Ibada Za Sanamu*. Na kisha nitawaambieni tokea hapo, kuhusu kama Bwana anaongoza kwa ajili ya ujumbe wa Krismasi, au la. Yaonekana kana kwamba nina ujumbe moyoni mwangu kwa ajili ya watu, wakati wa Krismasi. Basi nitawaambia tokea hapo.

<sup>82</sup> Sasa tuanze kusoma kwenye aya ya 12 ya sura ya 10 ya Yoshua.

*Ndipo Yoshua akanena na BWANA siku hiyo ambayo BWANA aliwatoa Waamori mbele ya wana wa Israeli, akasema mbele ya macho ya Israeli, Wewe Jua, simama kimya juu ya Gibeoni; na...Mwezi, simama katika bonde la Aiyaloni.*

*Ndipo jua likasimama, na mwezi ukatulia, hata hilo taifa lilipokuwa limekwisha jipatiliza juu adui wao. Hayo, je! hayakuandikwa ndani ya kitabu cha Yashari? Basi jua likasimama kimya katikati ya mbingu, wala halikufanya haraka kuchwa kama muda wa siku nzima. (Sikilizeni sasa.)*

*Haikuwapo siku nyingine mfano wa siku hiyo katika siku zilizotangulia mbele yake...wala katika hizo zilioandamana baada yake, hata ikawa yeye BWANA kuisikia sauti ya binadamu; kwa kuwa BWANA alipiga vita kwa ajili ya Israeli.*

*Basi Yoshua akarudi, na Israeli wote wakarudi pamoja naye, mpaka maragoni hapo Gilgali.*

<sup>83</sup> Mungu na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake. Sasa natamani, kama ni mapenzi ya Bwana, kwamba mtasubiri pamoja nami kwa dakika chache. Nataka kuchukua somo, geni, lisilo la kawaida; baada ya kusoma Maandiko kama hayo. Na nahitaji usikivu wenu na—na muombe wakati huu. Nataka kuchukua somo, la neno moja: *Kitendawili*.

<sup>84</sup> Na, kwanza, ningetaka kuelezea pengine kitendawili ni nini. Katika kamusi ya Webster, inasema kwamba *Kitendawili* linamaanisha “jambo ambalo haliaminiki, bali ni la kweli.” Hicho ni kitendawili. Jambo ambalo karibu haliwaziki, lisingeweza kuwa hivyo bali hata hivyo ndivyo lilivyo, hicho ni kitendawili. Sasa nataka nitulie dakika chache kwenye maneno haya, kitendawili.

<sup>85</sup> Sasa tuna mambo mengi ambayo tungeweza kuyataja kama kitendawili. Jambo moja ambalo ningetaka kutaja, ni, huu ulimwengu wenyewe ni kitendawili. Kusimama kwake ni kitendawili.

<sup>86</sup> Usiku uliopita nilikuwa ninazungumza na binti yangu, Rebeka, ambaye anasoma shule ya sekondari. Nami nilikuwa ninajifunza hapa kwenye Maandiko, na—na nilikuwa ninamwambia yeye kuhusu kusoma hii—aya hii hapa. Naye akasema, “Baba, Yoshua kwa kweli alisimamisha ulimwengu, sivyo?”

Nikasema, “Sijui ambacho alisimamisha. Yeye alisimamisha jua.”

<sup>87</sup> Akasema, “Asingeweza kusimamisha jua, kwa sababu jua halitembei.”

<sup>88</sup> Nikasema, “Nuru yake husafiri kuizunguka dunia, hata hivyo, basi alisimamisha hiyo.”

Akasema, “Vema, basi Mungu alisimamisha ulimwengu.”

<sup>89</sup> Nikasema, “Basi, kwa wale wasioamini kuna Mungu, nini kitakachotukia kama ulimwengu ukisimama na kupoteza nguvu zake za uvutano? Ungevurumika kwenye anga kama nyo—nyota, na vimondo vyake vingeaanguka kwa miaka mabilioni mia moja angani.”

<sup>90</sup> Bali Biblia ilisema kwamba, “Jua lilisimama, na kushikilia mahali pake siku nzima.” Naamini hilo. Naamini hilo. Ni la kipumbavu na haliaminiki, bali ni Kweli.

<sup>91</sup> Nawaomba mniambie basi, upande wa juu wa dunia ni upi, Ncha ya Kaskazini au Ncha ya Kusini? Unajuaje, kama uko angani? Unasema, “Ncha ya Kusini iko upande wa chini, chini yetu.” Wao wanafikiria Ncha ya Kaskazini iko upande wa chini, chini yao. Unaona?

<sup>92</sup> Imesimama angani, katika kijidua cha hewa, ikizunguka kwa mwendo wa maili elfu na kitu kwa saa. Sababu, kuna maili elfu ishirini na nne au ishirini na tano kuizunguka,

nayo hujizungusha katika masaa ishirini na manne, kwa hiyo inafanya iende zaidi ya maili elfu moja kwa saa, mzunguko. Na haikosei, inagonga sawasawa. Mahali ipo—mahali ipo kwenye ikweta ambapo inazunguka, haikosei hata dakika moja; inaweka saa kikamilifu, ikisimama angani. Kama hicho si kitendawili, sijui kitendawili ni nini. Jinsi ilivyo kwa taratibu zote za mbinguni, jinsi ambavyo zimeratibishwa vizuri, kikamilifu sana; hivi kwamba, katika miaka ijayo, miaka ishirini na thelathini tangu sasa, sayansi inaweza kuona kupatwa kwa jua na mwezi, zikipitana. Na yaweza ikuambie, kwa usahihi wa nukta, wakati ambapo zitapitana na kupatwa kutaanza lini.

<sup>93</sup> Hata saa tulizo nazo ziwe nzuri jinsi gani, mojawapo ya vyombo vyenye usahihi. . . Ninayo moja hapa ambayo nilipewa huko Uswisi, kama zawadi, nilipokuwa kule. Thamani yake ni kama dola mia tatu, katika fedha ya Kimarekani. Hiyo nilipewa. Hakuna juma ambalo haipaswi kurekebisha; saa zote, hakuna kitu anachoweza kuunda binadamu kilicho kikamilifu hivyo. Kitakuwa, mnamo miaka michache, kitachakaa hatimaye kiishe. Kadiri kinavyozeeka, kitazidi kuwa kibaya wakati wote. Johari zitachakaa. Usahihi wake utaondoka. Hakuna kitu ambacho kinaweza kuchukuliwa au kutengenezwa na binadamu, au kunolewa na binadamu, ambacho chaweza kudumu kikamilifu.

<sup>94</sup> Bali ulimwengu huu hudumu mkamilifu! Kitu gani kinauongoza? Vema, unasema, “Sijui kinachouongoza, ambacho kinaushikilia mahali pake.” Kweli jambo hilo ni kitendawili. Ni, huwezi kueleza jinsi Mungu anavyolitenda, bali Yeye hulitenda. Kwa hiyo, hilo ndilo jambo muhimu, kwamba Yeye hulitenda. Nasi twajua ndivyo ilivyo.

<sup>95</sup> Haiaminiki jinsi ambavyo ungeweza kuzungusha mpira angani, hautafanya mzunguko mmoja kamili ukiwa mahali pale pale.

<sup>96</sup> Nilikuwa ninafikiria, hapa siku moja, nilipokuwa kule nyikani. Na mojawapo ya jamii hii ya kale ya mipungate inayoruka ambayo asidi katika damu yako itaivuta kwako moja kwa moja, moja ya jamaa hao alinirukia. Nawe huwezi ukaiondoa, yakubidi uchukue kitu na uikwangu kuiondoa. Na ina vijimiiba vidogo juu yake. Na haidhuru utanoa sindano vema jinsi gani; sindano itakuwa butu nchani; mchongoko mkamilifu wa sindano utakuwa mkamilifu uwezavyo kuichonga, itakuwa butu, ukilinganisha na moja ya hiyo jamii ya mipungate inayoruka. Na hata hivyo ni jani, lenyewe, lililofingirishwa sana sana. Ingewezekanaje kwamba maumbile yangeweza kufingirisha jani likakazika sana na kuchongoka zaidi, nchani, kuliko mtambo mzuri sana ungeweza kunoa moja? Na, hata hivyo, kote hadi kwenye mwisho wa ncha ile ni vijimiiba vidogo kama ndoano namna *hiyo*, vijimiiba vidogo vya kulishikiza na kujishikilia lenyewe linapoenda. Loo, kitendawili, sawa, kwa sayansi. Haiaminiki, bali ni kweli.

<sup>97</sup> Ningetaka mtu fulani aeleze hili. Nisingeweza kukuambia maili hasa, au sayansi inasema ni maili ngapi kutoka duniani hadi mwezini. Bali jinsi gani mwezi ule, ningesema, ukisimama mamilioni na mamilioni ya maili toka duniani, na bado unaongoza maji kujaa na kupwa baharini. Nini kinafanya hivyo? Inawezekanaje? Ni kitendwaili, bali hata hivyo tunaangalia na kuona imetendeka. Inatukia. Mwezi huongoza maji kujaa na kupwa. Mwezi unapotikisika namna *hii*, wakati dunia, maji kujaa na maji kupwa hufuatana nao. Na Mungu ameweke mwezi utawale miendo ya bahari, na ameweke mipaka. Na haiwezi kuvuka mpaka ule ambapo Mungu amechora mstari, akasema, “Angalia, waweza kuja karibu mpaka *hapa*, bali huwezi kuchukua sehemu iliyobakia, kwani nimeweke mlinzi Wangu juu yako.”

<sup>98</sup> Nao mwezi, uko mamilioni ya maili toka duniani, huiita ile bahari, na kuweka mipaka yake na kuitawala. Haiaminiki! Kuna nini kule mwezini? Ambapo, maili chache tu toka duniani, uvutano wote, hewa yote, kila kitu, kinaondoka, unaenda nje kwenye anga ambako hakuna hata hewa, kwa mamilioni na mamilioni mara mamilioni ya maili. Na, hata hivyo, unaitawala! Kasema, “Unaweza kwenda umbali huo, bali huwezi kwenda mbali zaidi, kwani mimi ni mlinzi wa Mungu. Mimi ni mbwa mlinzi ambaye huketi hapa, na huwezi kupita mipaka *hii*.” Eleza hilo. Hicho ni kitendawili, jinsi ambavyo Mungu hufanya hilo, bali hata hivyo Yeye hulitenda. Haielezeki.

<sup>99</sup> Tuna majira ya kipupwe, theluji ardhini, baridi, ardhi inaganda. Mbegu ndogo, na katika mbegu hiyo ndogo kuna chembe ya uhai, na mbegu hiyo ndogo itaganda na kupasuka, nao mseto utaitoka. Na hiyo chembe ya uhai itakaa mavumbini, kwenye utando wa barafu ambao ungeangamiza uhai wote. Unahifadhiwaje, hata ukachipuka tena katika majira ya kuchanua? Tusingeweza kuelezea hilo, sivyoy? Ni kitendawili.

<sup>100</sup> Tunachukua Waebrania, sura ya 11 na aya ya 3, tunaielewa hapo kwamba Biblia inasema, Paulo akinena, kwamba, “Ulimwengu uliumbwa na kufanyizwa kwa Neno la Mungu,” kitendawili, ambapo Ne—Neno lingetamka na kutokana na Neno hilo kunge—kungetengenezwa vitu vinavyoonekana, “Yaani vitu ambavyo ni dhahiri vilitengenezwa kwa vitu ambavyo si dhahiri.” Vitu ambavyo tunaona, vilikuwa Neno lililonenwa la Mungu. Dunia ni Neno la Mungu. Miti ni Neno la Mungu. Kwa nini tuogope kumwamini Mtu ambaye ametoa Neno kama hilo, kwa Uweza wa namna hiyo pamoja na mamlaka? Kwa nini tuogope kuchukua Neno hilo kwa ajili yetu na kulitumia Hilo sisi wenyewe? Inaonyesha tulikoangukia, katika kutokuamini. Neno, Neno la Mungu, kitendawili! Kweli ni kitendawili, Neno la Mungu.

<sup>101</sup> Pia, ningetaka kuonyesha kitendawili haraka sana, na hicho ni hapo Mungu alipomwita Ibrahimu akamwambia, alipokuwa

na umri wa miaka mia moja; na Sara alikuwa tisini, miaka arobaini kupita wakati wake wa kupata hedhi. Naye Ibrahimu, ambaye uhai wake ulikuwa kama mfu; na Sara, aliyekuwa tasa kwanza, na tumbo lake la uzazi kama lililokufa. Hata hivyo Mungu alisema kwamba Yeye atamleta, kupitia kwao, mtoto. Jambo hilo ni kitendawili. Muulize daktari kama mwanamke, umri wa miaka mia moja, angeweza kulea mtoto, kupata mtoto. Haiwezekani, haliaminiki, bali alizaa kwa sababu Mungu alisema angefanya jambo hilo.

<sup>102</sup> Ni jambo lisiloaminika, kufikiria mtu angeweza kuketi huku mgongo wake umeelekezwa kwenye hema, mgeni aliyejaa vumbi nguoni Mwake, na amwambie mwanamke, aliyekuwa nyuma ya lile hema, alilokuwa anafikiria. Kitendawili, haisadikiki, bali hata hivyo ni kweli.

<sup>103</sup> Haikusadikika, wakati Ibrahimu alipomchukua Isaka juu mlimani, mwanawe wa pekee, akamchukua hadi kwenye kilele cha mlima, kumtoa sadaka. Na alipofika juu ya mlima, na akamlaza Isaka juu ya kuni, huku akiwa tayari kuutwaa uhai wake. Basi alipokuwa anashusha mkono wake, Kitu fulani kiliushika mkono wake! Na palikuwa na kondoo dume ambaye pembe zake zilinaswa, huko nyikani, mlimani. Kitendawili! Yule kondoo dume alitoka wapi? Ingewezekanaje awe maili mia toka kwenye ustaarabu, bila ya kuuawa; huku kuna simba na—na mbweha, mbwa mwitu na wanyama, na kadhalika? Alitoka wapi? Alipataje kuwa pale, kule juu ya mlima ambako hakuna maji? Kwa nini hakuwepo pale alipokuwa anaokota mawe? Alipaita *Yehova-Yire*, “Bwana amejipatia Mwenyewe sadaka.” Haisadikiki bali hata hivyo ni kweli kabisa, kwani Yeye ni *Yehova-Yire*. Mambo yasiyosadikika kwenye ujuzi wetu na sayansi, bali hata hivyo ni kweli! Kitendawili kikuu!

<sup>104</sup> Ilikuwa kitendawili, na itakuwa hivyo, wakati Yesu, Marko 11:22 na 23, Yeye aliposema, “Kama ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, ila uamini kwamba hayo uliyosema yametukia, yatakuwa yako.” Halisadikiki, bali ni kweli. Ni kitendawili.

<sup>105</sup> Hebu nisimamie hapa niseme, huko msituni, nikiwa nimeketi kando ya mti ule asubuhi ile, hakuna kindi mwituni, bali Sauti iliponena na kusema, “sema watakuwa wapi.”!

<sup>106</sup> Na hapo, hivyo anisidie, kama nikifa kabla ya kumaliza ujumbe huu, huku nikielekeza kidole changu kwenye mlozi usio na majani, nilisema, “ataketi pale *pale*,” na hapo akawepo! Haisadikiki, bali ni kweli!

Yeye akasema, “Anayefuatia atakuwa wapi?”

<sup>107</sup> Nikasema, “Kule kwenye tita lile la kichaka na vinginevyo,” na kabla sijawahi kushusha kidole changu huyo hapo!

“Anayefuatia atakuwa wapi?”

108 “Toka penye gogo lile kwenye shamba lile.” Na huyo hapo akatokea! Haisadikiki.

109 Nilimuuliza mke wangu, juzijuzi asubuhi. Nikasema, “Mpenzi, hivi nimepotewa na akili zangu? Ninaanza kuwa mwenda wazimu? Hivi nina nini? Kwa nini ninasema mambo ninayoyasema? Kwa nini ninafanya mambo ninayoyafanya? Nini kinachonifanya?” Ninawapenda watu, hata hivyo ninawararua vipandevipande. Nami ninafunga na kuomba niliondoe kwangu; na kadiri ninavyofunga na kuomba, ndivyo inavyozidi kuja zaidi. Haisadikiki, bali ni kweli! Ni kweli.

110 Nilimwona mwanamke akiinua mkono wake saa hiyo, nyuma huko jengoni, akimsifu Bwana. Huyo alikuwa ni Hattie Wright, akiketi chini kule. Wakati, alikuwa na wavulana wawili, kama watanisamehe mimi nikinena hili, watukutu, wavulana wa kilimwengu. Maskini mwanamke huyu akiwa ameketi pale siku ile, mjane. Nami nilisema, “Hattie, Bwana Mungu... ulisema neno linalofaa. Yeye alitoa wale kindi. Yeye ni Yehova-Yire.”

111 Yeye akasema, “Jambo hilo si kitu kingine bali kweli tupu ya Mungu!” Loo, alisema neno linalofaa! Inaonekana isiyosadikika kwamba binadamu angeweza kusema neno. . .

112 Kama vile Ndugu Booth alivyowaambia. Jinsi tulivyo wachafu na waovu, ni Nani Yule aketiye huko ng’ambo ya mwezi na nyota, na anga lote na wakati na Umilele? Kama hata Booth alivyolinena hilo, nami nilisoma jambo lile lile hivi majuzi, nikisoma habari za Ireneo, kwamba hata Malaika ni wachafu machoni Pake. Sisi ni nani?

113 Lakini mwanamke alisema jambo lifaalo, ambalo huuita moyo wa Yehova! Akasema, “Muulize anataka nini, kisha umpe hicho.” Amina. Halisadikiki, bali ni kweli! Papa hapa sasa na mbele ya macho yetu kuna uthibitisho wa kuonekana, aliomba nafsi za watoto wake wa kiume wapate kuwa Wakristo. Mungu akampa haja yake. Halisadikiki! Huo ulikuwa muujiza mkuu kuliko kuponywa mgonjwa. Hiyo ni kubadili maisha ya mtu, nafsi yake, mwili, na vyote alivyo. Ilibadilisha maumbile yake. Haisadikiki, bali ni kweli! Kilikuwa kitendawili. Tunaliona hilo kila mahali.

114 Kitendawili katika zamani za Nuhu. Wakati, Nuhu, mtu, mtu wa kawaida tu, akawa nabii, au alikuwa nabii wa Bwana, labda alikuwa mkulima. Mungu alimwambia, “Jiandae kwa ajili ya mvua itakayoshuka kutoka Mbinguni,” wakati hapakuwepo na mvua. Hapajakuwa kamwe na mvua. Hakuna njia ya kupata mvua juu kule. Haikuwahi kunyesha duniani. Hapakuwa na bahari, hapakuwa na maji, bali bado Mungu alimwambia ajenge safina nyumba yake ipate kuokolewa. Basi Mungu akaileta mvua. Ilikuwa ni kitendawili. Si jambo la kisayansi, bali (nini?) ilikuwa kitendawili, kwa vyo vyote. Ndiyo.

<sup>115</sup> Ilikuwa kitendawili wakati wale wana wa Kiebrania ambao walikuwa wameamua kudumu katika Neno la Mungu, haidhuru nini kimetukia, kwamba mfalme alijenga lile tanuru litoe moto mara saba zaidi kuliko lilivyowahi kuchochewa moto, na kuwatupa watu wale mle ndani. Wakati, joto kali sana la—la tanuru liliwaua watu waliotembea kwenye daraja la kuingilia mle pamoja nao, kwenye mdomo wa tanuru, hao walikufa. Bali hata hivyo watu wale walitembea mle tanuruni kwa pengine masaa matatu. Kusingebakia hata na vumbi lao, kwa kuwa uhai wa kibinadamu uliokuwemo ndani yao ungeangamia. Iwapo lilifanya uhai wa binadamu mmoja upotee, kwa kulikaribia, lingetenda nini kwa uhai wa binadamu mwingine? Bali waliwatupa mle ndani, na tuseme masaa matatu, huenda ikawa yalikuwa matano.

<sup>116</sup> Huenda ikawa alikwenda akala chakula cha mchana, na kurudi, akasema, “Fungua mlango wa tanuru. Hakutakuwa hata na vumbi lao hao watu lililobakia!” Bali alipofungua mlango, hao hapo, hawakudhurika, wakitembea huku na huko motoni. Haisadikiki, bali ni kweli! Kwa nini? Yeye alisema, “Mliweka wangapi mle ndani?”

Wakasema, “Tumeweka watatu ndani.”

<sup>117</sup> Akasema, “Naona wanne.” Hilo ndilo lililofanyiza kitendawili. “Na Yule pale anaonekana kama mwana wa miungu.” Hakuwa mwana wa miungu; Yeye alikuwa Mwana wa Mungu! Wao walikuwa wapagani. Loo, Mungu ndani ya Neno Lake kuu!

<sup>118</sup> Kulikuwa na wakati ambapo jeshi la Mungu liliona woga hata likamwogopa mtu, nalo likasimama kwenye mtelemko wa kilima. Walipomwachilia mtu mmoja ambaye alikuwa mara tatu ya kimo cha ye yote kati yao, asimame kule nje kwenye mtelemko wa kilima, na kusema, “Sasa mnamtegemea Mungu wa kweli, mnasema. Ama, mmoja wenu ninyi jamaa atoke aje apigane nami, na hatuta—hatutakuwa na kumwaga damu kwo kwote.” Adui wa Mungu alilrudisha nyuma kanisa la Mungu kwenye mtelemko wa kilima, nao walikuwa wakilikubali! Walikuwa wanaogopa. Walikuwa waoga.

<sup>119</sup> Na hapo maragoni kikaja kijitu kidogo, kimejizungushia kijingozi cha kondoo mwilini, koti la mchungaji; mtu mdogo sana katika jeshi lote, na hata si askari. Bali ilikuwa kitendawili, Mungu alipomchukua huyo mtu mmoja, maskini jamaa yule mmoja asiyehusika. Biblia ilisema alikuwa mwekundu. Kijitu hicho kimoja kilifukuza jeshi lote, yule adui! Jambo hilo lilikuwa ni kitendawili. Ilionekana kana kwamba Mungu angelipa hilo jeshi kuu linalotembea kwa miguu, moyo wa kwenda vitani. Walikuwa watumishi wa Mungu, kwa nini wasiende wakapigane vita vya Mungu? Huyu ni adui wa Mungu, ichukueni! Inaonekana

kama Yeye angewapa ujasiri. Bali Mungu alichukua kijitu kimoja.

<sup>120</sup> Pia kumbukeni, kitendawili kingine, hakuchukua upanga kamwe. Sauli alijaribu kumvisha silaha zake, akajaribu kuweka upanga mkononi mwake. Maskini kijitu kile hakikuweza kuushika. Basi akachukua kombeo, mpira mdogo au ngozi ndogo, na vipande viwili vya kamba vimefungiwa kwake. Naye akalishinda jeshi zima la adui, akawafukuza. Ilikuwa kitendawili, jinsi maskini mvulana huyo mmoja mdogo alivyoweza kulifukuza jeshi.

<sup>121</sup> Ni kitendawili. Hakika. Mungu hulitenda. Yeye amejaa vitendawili. Hakika, ndivyo alivyo. Hilo ndilo atendalo. Ndivyo Yeye anavyotenda mambo. Ndiyo, bwana. Jambo hilo lilikuwa kitendawili.

<sup>122</sup> Misri ilipokuwa na jeshi kuu walilokuwa nalo, ulimwengu mzima ulishindwa. Walitawala kila taifa. Na wakati Mungu alipoamua kuharibu jeshi lile, kuharibu taifa lile, ilionekana kama Yeye angeinua jeshi la Waamori, au jeshi fulani kuu mahali fulani, naye awapeleke chini kule wakiwa na zana zao nzuri zaidi; au angeunganisha madhehebu yote pamoja, kushuka kwenda kupigana, pamoja, kusudi apate ushirikiano kamili. Bali, Mungu alitumia kitendawili! Alichukua mwanamume mzee, mwenye umri wa miaka themanini, na hakuweka kamwe upanga mkononi mwake, bali fimbo iliyochakaa na iliyopindika, hiyo ikaizamisha Misri chini ya bahari ya chumvi. Halisadikiki, ambalo Mungu anaweza kufanya, bali hivyo ndivyo Yeye anavyofanya mambo. Yeye hutumia vitendawili kufanya jambo hilo. Unaona, Yeye hulifikisha kwenye kitendawili, fimbo iliyopindika ya mchungaji badala ya jeshi la miguu, kushinda ta—taifa ambalo liliutawala ulimwengu.

<sup>123</sup> Loo, jambo pekee Mungu analingojea sasa hivi, ninaamini. Urusi haimaanishi kitu kwa Mungu. Yeye anataka kupata mtu mmoja. Si lazima awe na mashirika makubwa. Si lazima awe na madhehebu makubwa. Yeye anataka apate mtu mmoja ambaye Yeye anaweza kumzungushia Roho Wake ndani yake! Hilo litasimulia yaliyosalia, patakuwepo na kitendawili kingine, hata Yeye awezapo kumpata mtu fulani aliyejitolea kikamilifu, hilo litatenda jambo hilo. Hivyo ndivyo Mungu anavyotenda kazi Yake, Yeye hutumia vitendawili.

<sup>124</sup> Ilikuwa kitendawili wakati askari mkuu wa—wa Mungu, jina lake Yehoshafati, aliposimama malangoni, na mtu aliyerudi nyuma jina lake Ahabu, akasema, “Kabla ya kwenda kupigana vita hivi, je, si jambo jema kwamba tutake shauri kwa Bwana?” Sasa, iwapo moyo wa mtu yule una njaa, kujua mapenzi ya Mungu, lazima yapo mapenzi ya Mungu mahali fulani.

<sup>125</sup> Si kila wakati ambapo kuna usalama katika wingi wa ushauri. Ahabu anasema, “Ninao wahudumu wangu wote.

Wote ni manabii. Nitawaita hapa. Nawe unajua, kama nikileta manabii mia nne, tutapata Neno la Bwana.” Si sikuzote unaona, si sikuzote.

126 Kama haiambatani na Neno, basi jitenge na jambo hilo. Sijali wako wangapi hapo. Dumu katika hilo Neno! Mungu hawezi kughairi Neno hilo.

127 Sasa, aliwaleta wote hapo, na wote wakatabiri kwa moyo mmoja, kwamba, “Bwana alikuwa pamoja nao. Kweeni!”

128 Bali bado kulikuwa na kasoro fulani. Na yule mtu wa Mungu alijua hilo halikuwa sahihi. Akasema, “Hamna mwingine zaidi? Mwingine tu, mahali fulani?”

“Loo,” akasema, “tuna mmoja, bali ninamchukia.”

Akasema, “Hebu mfalme na asiseme hivyo.”

129 Mungu alimchagua mvulana mmoja asiyejua kusoma, aliyeonekana kidogo mhaini kwa taifa, mtu aliyedharauliwa na kukataliwa, kuleta ujumbe Wake kwa mwenye moyo wenye njaa. Na badala ya madhehebu yote pamoja kunena kwa moyo mmoja katika umoja, Mungu akaleta mtu mmoja. Kitendawili, bali mtu huyo anayo Kweli. Na ilithibitika kuwa Kweli, kwa sababu yeye alishika Neno. Jambo hilo lilikuwa kitendawili, kweli kabisa.

130 Sasa unasema, “Una maana hukubaliani na *hili* lote na *lile*, na *lile*?” Kama halichukواني na Neno, sikubaliani nalo. Hiyo ni kweli. Neno la Mungu halitashindwa kamwe.

131 Nilipokuwa nikizungumza na kasisi, si muda mrefu uliopita, alisema, “Bw. Branham, unajaribu kubishania jambo fulani kutokana na Biblia.” Kasema, “Sisi tunaamini kanisa, hatuamini lingine ila hilo. Tunaamini kanisa, kanisa lisemayo. Mungu yuko katika kanisa Lake.”

132 Nikasema, “Mungu yumo katika Neno Lake. Na Yeye ni Neno.” Hilo ni kweli, Neno!

133 Hiyo ndiyo sababu Mikaya alichukua Neno. Kisha Mungu akatumia kitendawili kutahayarisha kila madhehebu, na akalitimiza Neno la mtumishi wa Mungu; mtu mmoja, aliyedharauliwa, aliyekataliwa, aliyechukiwa! Nini? Aliyechukiwa na watu wake mwenyewe. Naam, hakuwa mkomunisti, au hakuwa kitu kingine. Hebu tuseme yeye alikuwa ni mpentekoste, nayo makundi ya Kipentekoste yakamchukia yeye. Hayakumpenda. Hawakumjali. Lakini alikuwa na Neno la Mungu. Mungu alitunga kitendawili kutokana na jambo hilo.

134 “Kwa nini Yeye asingekubaliana nao, kama wote hawa ni manabii na wahudumu, na kadhalika, kwa nini isiwezekane, katika kundi lote hili kubwa, kuamua jambo bora zaidi kuliko mtu mmoja? Yaonekana si busara kwamba Mungu angefanya tu Neno la mtu mmoja sahihi, kuliko la hao wengine.”

<sup>135</sup> Kwa sababu, neno la mtu yule lilikuwa Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu Mungu alitekeleza jambo lile, kwa sababu yule mtu alishika Neno la Mungu. Wale wengine walikuwa wanatabiri uongo. Ndiyo, ilikuwa kitendawili hapo Mungu alipochukua Neno la mtu mmoja mdogo, na kulifanya kweli, kwa sababu lilikuwa ni Neno Lake. Yambidi Mungu asimame na Neno Lake, si neno la halmashauri. Bali, Neno la Mungu, huyo ndiye ambaye Yeye husimama naye.

<sup>136</sup> Alimchukua Mikaya badala ya shule nzima ya wahudumu waliofunzwa vizuri sana, watu wenye sifa. Sina neno dhidi yao, wao walikuwa watu mashuhuri. Walikuwa watu ambao hawakuamini katika Mungu mwingine, walimwanimi Mungu yeye yule ambaye Mikaya alimwamini. Lakini walitenda kana kwamba waliamini Hilo, bali hawakuliamini Neno Lake. Kwa sababu, walitaka kupendwa na watu. Walitaka kujipendekeza kwa mfalme. Na upofu wao ulipuuza Neno la kweli la Mungu. Je! Mungu angeweza kubariki kitu ambacho Yeye amelaani?

<sup>137</sup> Enyi mabibi na mabwana, nyote, msifikiri kwamba ninatenda hili kwa chuki. Ninalitenda kwa uaminifu. Hiyo ndiyo sababu yake. Naweza kusema kwamba, “Wanawake wangepaswa kuwa...vema, basi na wakate nywele zao, na mambo kama hayo; wavae, nguo zao, hilo halihusiani na Jambo hilo”? Neno la Mungu linasema linahusiana! Amejaa fedheha na aibu maadamu analitenda, naye Mungu hatajishugulisha naye kamwe. Sijali kiasi gani ananena kwa lugha, au anaruka au anapaza sauti, hajafikia po pote kwa Mungu, bado. Hilo ni Neno la Bwana.

<sup>138</sup> Mwanamume, wewe ambaye huwezi kutawala nyumba yako mwenyewe, halafu mnajaribu kuwa wahubiri na mashemasi? Unafaa vipi kuwa mhubiri kwenye mimbara, kuongoza Kanisa la Mungu aliye hai, na kuwagawia urithi wao? Wakati ambapo, unawazia zaidi kuhusu riziki yako na sadaka unayopata kuliko unavyowazia Neno la Mungu, na kuona haya kulinena mbele ya wanawake, unaogopa hutapendwa na watu. Mungu na airehemu nafsi yako yenye dhambi!

<sup>139</sup> Nena Neno la Mungu, katika Kweli! Yohana alisema, “Shoka limewekwa kwenye shina la mti.” Nalo hilo shoka ni Neno la Mungu. “Kila mti usiozaa matunda yafaayo, ukate ukautupe motoni.” Mungu, tulettee kitendawili kingine!

<sup>140</sup> Kwa nini Mungu alimchukua Yohana Mbatizaji, kama nilivyokuwa nikizungumza sasa hivi tu, badala ya makuhani Wake waliofunzwa vizuri wa zamani hizo? Alichukua mtu ambaye hajawahi kwenda shuleni hata siku moja maishani mwake. Kwa hiyo, tunafahamu kwamba Yohana alienda nyikani, mwenye umri wa miaka tisa, na alikuwa peke yake na Mungu.

<sup>141</sup> Siku chache zilizopita, katika kusoma kuhusu Baraza la Nikea. Hiyo ilikuwa ni muda mrefu baada ya kifo cha mtume

wa mwisho, Mtakatifu Yohana. Wakati watu hao walipokuja pale kwenye lile Baraza la Nikea, baadhi ya hao ndugu wazee waliwatahayarisha hao wengine. Walikuja pale, wamevaa ngozi za kondoo; kwa wale wafalme waliovalia majoho, kama Konstantino na maaskofu wa Rumi. Wamejizungushia ngozi za kondoo zilizochakaa, nao waliishi nyikani, wakila mboga, bali walikuwa manabii wa Bwana. Kanisa lile dogo, upande wa Kiyunani, liliendelea; upande wa Warumi ulirudi nyuma. Lakini hiyo inaonyesha, unapopatana, huwezi kuwa mtumishi wa Kristo.

<sup>142</sup> Yohana. Katika siku hiyo, kanisa lilikuwa la kidehuri sana, walikuwa na makasisi, watu waliofundishwa vyema. Bali Mungu alimchagua mtu ambaye hakuwa na elimu hata kidogo, na akamchukua kutoka nyikani, huku amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, na masharafa yake yote yakiwa yametokeza, nywele zake zikining'inia shingoni mwake. Hakuna mimbara ya kuhubiria. Hakuna kanisa la kumkaribisha. Ila labda alisimama kwenye matope, yameifunika miguu yake hata magotini, naye alihubiri, "Ufalme wa Mungu umekaribia!" Mungu alimchagua mtu yule.

<sup>143</sup> Yesu aliposema, "Mlitoka kwenda kumwona nani, mtu ambaye anaweza kuzungumza kwenye shule zote hizi, mtu ambaye amevalia mavazi mororo, na kadhalika?" Akasema, "Wako kwenye majumba ya wafalme." Kasema, "Mlitoka kwenda kumwona nani, nabii?" Akasema, "Zaidi ya nabii. Huyu ndiye ambaye nabii alinena kwamba atakuja, 'Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.'" Yeye alikuwa malaika wa agano. Alikuwa m—mtangulizi mkuu.

<sup>144</sup> Ila, ilikuwa kitendawili, jinsi ilivyotendeka. Kwa nini Yeye hakuja kwenye shule ile kubwa juu kule Yerusalemu? Kwa nini hakuja kwa Kayafa, kuhani mkuu? Kwa nini Yeye hakuja kwa baadhi ya wale watu mashuhuri, waliofunzwa, ambao walifunzwa tangu utoto wao, baba zao waliofunzwa kabla yao, na baba zao waliowatangulia, kwa kizazi baada ya kizazi baada ya kizazi, wamefunzwa na kuelimishwa, watu wazuri, waliostaarabika sana, walioelimishwa? Na basi aokote mwanamume kizee toka nyikani, ambaye kamwe hajawahi kupata mafunzo ya shuleni hata siku moja maishani mwake, na amweke nje huko Yordani, na aseme, "Huyu, mtu huyu ndiye." Kitendawili, bila shaka. Halisadikiki, bali ilikuwa kweli. Mungu alitenda jambo hilo.

<sup>145</sup> Kuzaliwa kibikira kwa Bwana wetu, haisadikiki, kwa mwanamke kuzaa mtoto bila ya kumjua mwanamume. Mungu alitenda jambo hilo. Mungu alifanya hivyo. Unaona, ni kitendawili. Akamchukua maskini mwanamke kizee chini kule, maskini msichana mdogo, amechumbiwa na mwanamume mwenye umri wa miaka kama arobaini na mitano, yeye mwenyewe alikuwa na kama miaka kumi na sita au kumi

na minane, na akachumbiwa na mwanamume huyu ambaye alikuwa mjane, wa watoto wanne. Ndiposa akamchukua mwanamke huyu akamfunika kama kivuli kwa Roho Mtakatifu, naye akachukua mimba tumboni mwake ya mwili ambao ulifanya maskani ya Mungu Mwenyezi. Kitendawili!

<sup>146</sup> Jinsi ambavyo Yeye hawezi kutoshelea Mbinguni! Dunia ni mahali Pake pa kuwekea miguu, Mbingu ni kiti Chake cha enzi, na hata hivyo aliweza kuleta utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, na kuuweka Huo katika Mwanadamu. Loo! Wakati, unaweza kupima kwa mamia ya mabilioni ya maili kwenye utitiri wa wakati, na kamwe usimpime Mungu; hata hivyo kitoto kichanga, huku kimelala kwenye hori, kilijawa na utimilifu wa Uungu Wake kwa jinsi ya mwili. Yehova! Kitendawili! Yule Mungu mkuu, Ambaye huketi nyuma kule, kutawala jua milioni mia moja zinazowaka kwenye sayari, ambaye hana mwanzo kamwe wala kamwe hana mwisho, na angejitwika mwili, kwenye hori lenye samadi!

<sup>147</sup> Halafu tunatoka na kucheza dansi na kunywa, na kufanya yasiyofaa, katika tafrija! Si tafrija; ni ibada! Tunaadhimisha Krismasi. Jinsi ambavyo Mungu alitenda hilo, ili Yeye apate kufa, kupachukua mahali pa mwenye dhambi.

<sup>148</sup> Ilikuwa ni kitendawili wakati mvulana mdogo, aliye na nywele za kipilipili, kijitu chenye mabega yaliyoinama, labda hakufikia urefu wa futi tano; naye alikuwa na vishungi saba vya nywele vilivyoning'inia chini kuzunguka kichwa chake, maskini dondoandume. Naye alikuwa njiani akienda, siku moja, kumwona mpenzi wake, ndipo simba akamngurumia.

<sup>149</sup> Hivi kuna mtu amewahi kusikia mlio halisi wa simba? Labda uliwahi kusikia, katika hivi vizimba na kadhalika hapa. Bali nataka kukuambia, hao wanalia tu wakati huo kama paka. Yakubidi kusikia wa mwituni hasa akinguruma. Miamba itaanguka toka kilimani, umbali wa nusu maili; vijiwe vidogo vitaporomoka chini ya kilima, huitingisha tu ardhi namna hiyo. Mngurumo huo unakotoka, sijui.

<sup>150</sup> Loo, nilimwona mmoja, siku moja, alikuwa anainamisha kichwa chake chini, simba dume mkubwa mzee mwenye nywele za manjano shingoni alimngurumia mmoja mweusi, kwa sababu, mwenye nywele nyeusi shingoni, kwa maana alikuwa ameokota kipande cha nyama. Alikiacha kimekaa hapo, na yeye ni kama tu aliyesema, "Sasa usiguse hicho, ninashuka kwenda kunywa maji." Naye akashuka kunywa maji kwa ulimi. Aliporudi, huyu mwenye nywele nyeusi shingoni alikuwa anakilamba. Yule baba mzee akasimama tu, akakiinamisha kichwa chake chini, na akatoa mlio wa kutisha sana, na, nasema, kwamba miamba iliporomoka kilimani. Loo, jamani! Angelitikisa jiji hili, kama angenguruma namna hiyo hapa. Mngurumo wa simba, loo, unatisha sana!

<sup>151</sup> Na mngurumo huo ukakikabili hiki kijitu chenye nywele za kipilipili, tungemwita hivyo, na jambo fulani likatukia. Hicho kijitu kikasogea mbele na kumshika kinywani, na kuweka mkono mmoja chini namna *hii* na mmoja ndani namna *ile*, bila wasiwasi, na kumpasua tu na kumweka hapo chini. Jambo hilo ni kitendawili. Nini kililisababisha? Kama ungeangalia maneno yaliyotangulia hilo, “Na,” kile kiungo “Roho wa Bwana akamjia.” Hilo ndilo lililoleta tofauti. Naye akamuua yule simba.

<sup>152</sup> Basi siku moja Wafilisti walikuja kumfuatilia. Alikuwa hana silaha. Walikuwepo elfu moja. Walikuwa na mikuki mirefu na ngao kubwa, na hiyo ni kama mlango mbele yako, namna *hiyo*, zile ngao. Wazia tu ngao kubwa, kubwa mno ya shaba nyeupe sasa, toka juu hata chini mbele yako, na wamevaa chapeo za shaba nyeupe, makoti makubwa ya shaba nyeupe, na kila mahali kwenye miundi na kila kitu, cha shaba nyeupe; mikuki mikubwa mno na mirefu, mirefu kama hizo inayofikia hadi kwenye nguzo ile kule, urefu wa futi kumi na tano, ishirini. Chapeo kubwa za shaba nyeupe kichwani namna hiyo, kali kama wembe. Basi wakakiona kijitu hiki chenye nywele za kipilipili kinashuka kutoka Palestina, kumtembelea mpenzi wake fulani chini huko. Kwa hiyo wakasema, “Kile pale kile kijitu. Twende tukakichukue mateka!” Mtu mmoja angeweza kumchukua kwa ncha ya mkuki ule, kumwinua tu juu na kumtikisa kidogo, naye angeangukia moja kwa moja mkononi mwake, aangukie kishikio cha mkuki ule. Mbona, chenyewe ni maskini kijitu kidogo tu.

<sup>153</sup> Baadhi ya watu, wasanii, wakijaribu kumchora Samsoni akiwa na—akiwa na mabega asingeweza kuingia kwenye Maskani hii. Naam, hilo lisingekuwa la ajabu, mtu mkubwa namna hiyo. Samson alikuwa maskini jamaa mdogo tu, bali Roho wa Bwana ndiye aliyekuwa mkubwa. Unaona? Yeye huchukua ile... Hilo—hilo—hilo ni kutoyaheshimu Maandiko, kusema alikuwa mtu mkubwa namna hiyo.

<sup>154</sup> Mungu siku zote huchukua vitu vipumbavu na vijinga kama hivyo, apate kuvitumia kufanya kazi Yake, unaona. Yeye huchukua kitu ambacho ni bure.

<sup>155</sup> Kwa hiyo huyu jamaa mdogo alikuwa amesimama nje huko, mara hawa hapa Wafilisti wanakuja na kumzunguka, ili wamuue. Naye akatwaa mfupa wa taya la nyumbu ambao ulikuwa pale, wa mwituni, punda mdogo, akautwaa ule mfupa wa taya la nyumbu yule. Nayo Roho ya Bwana ikamjia. Na hapo pakawa na kitendawili, jinsi ambavyo aliwapiga hata akawashinda, kwa mfupa wa taya la nyumbu, kupenya ile chapeo yenye unene wa nusu inchi utosini, kwa mfupa wa taya la nyumbu! Mbona, kwanza, mfupa ule mkavu wa siku nyingi uliokuwa pale, kwa pigo la kwanza, ungepasukapasuka katika vipande elfu, juu ya moja ya zile chapeo au zile ngao kubwa.

Ambapo, elfu walipomvamia, alimpiga kila mmoja wao mpaka akafa. Kitendawili! Hapo ndipo Roho ya Mungu ilipomjilia.

<sup>156</sup> Loo, laiti tungelikuwa mifupa ya taya la nyumbu katika mkono wa Mungu, kungekuwepo na kitendawili kingine. Ndiyo, ilikuwa hivyo.

<sup>157</sup> Ilikuwa kitendawili wakati Yesu Bwana wetu alipochukua biskuti tano na samaki wadogo wawili, na kuwavunjavunja, na akawalisha elfu tano. Na wakaokota vikapu vilivyojaa masalia, vifurushi vidogo ambavyo baadhi yao hawakula. Wakaweka samaki wanne au watano katika meza *hii*, na mikate minne au mitano, halafu wakaenda *hapa* na kuweka mikate minne au mitano. Na baadhi yao hawakuweza kula wakavimaliza, waliviacha tu pale. Kwa hiyo waliviokota, vikapu vilivyojaa vitu hivyo. Loo! Unaona? Yeye alifanyaje hilo? Halisadikiki kwamba Mtu angechukua biskuti tano na samaki wadogo wawili, na kuwalisha elfu tano, na kuokota vikapu saba vilivyojaa, mabaki. Halisadikiki, bali Yeye alilitenda. Kwa nini? Ilikuwa ni Mungu. Ilikuwa kitendawili. Halisadikiki, bali Yeye alilitenda.

<sup>158</sup> Lilikuwa halisadikiki, na kamwe hapo kabla au baadaye, kwenye bahari yenye dharuba, na mawimbi makubwa sana hata yalikuwa yanazamisha ile meli, wakati Mtu alipokuja anatembea juu ya hayo mawimbi. Naweza tu kuona kila wakati yale—lile wimbi kubwa lenye povu likija na kumzunguka Yeye, linapasuka tu na kuanguka chini, Naye anaendelea mbele, kama tu kwamba Yeye alikuwa anatembea juu ya kipande cha saruji. Akitembea juu ya bahari, katika wakati wa dharuba! Hebu sayansi na iwazie jambo hilo. Nini kilimshikilia Yeye juu hapo? Nini kilimshikilia juu ya bahari ile, ambapo pana kina cha nusu maili papo hapo? Wakati hayo mawimbi makubwa, makubwa mara nyingi zaidi kuliko Maskani hii, yakirusha maji, kwa nini, kwa nini, yalijaza ile mashua ndogo na kuilowanisha kwa maji. Ilikuwa imelowa ndani na nje, nayo inazama, milingoti imekwisha vunjika, na makasia hayapo, na matumaini yote ya kuokolewa yamekwisha. Na hapa yuaja Mtu akitembea juu ya maji! Kitendawili, hakika, halisadikiki, haliwezekani kuelezewa, bali Yeye alilitenda. Loo, ndiyo, Yeye alilitenda, akaja anatembea juu ya maji. Haisadikiki kwamba Mtu yuyu Huyu...

Ee Mungu, natumaini hili litafahamika!

<sup>159</sup> Halisadikiki, kitendawili kwelikweli, kwamba Mtu yuyu huyu, Yesu wa Nazareti, angechagua kundi la wavuvi wasio na elimu kuwa Kanisa Lake, badala ya makasisi waliofunzwa vizuri na madhehebu ya zamani zile. Jinsi ambavyo Mungu ambaye ni mwenye hekima yote, ambaye aliweza kutembea juu ya maji, ambaye angeweza kugeuza maji kuwa divai, ambaye aliweza kuchukua biskuti tano na kuwalisha watu elfu tano, na kuokota vikapu saba vilivyojaa mabaki! Jinsi ambavyo Mtu yuyu huyu,

Mungu aketiye kule ng'ambo katika Umilele, ambaye anang'ara sana hata jua humficha Yeye nyuso zao; kisima hasa cha hekima na usafi, na cha ufahamu na maarifa, Mkuu wa wakuu! Na Yeye angekuja katika mahali ambapo madhehebu makubwa ya makanisa yamekusanyika pamoja na yamewafundisha watu wao wote, Naye angeshuka na kuokota kundi la wavuvi wachafu, na wanaonuka ambao hata hawangeweza kuandika majina yao wenyewe, na kuchagua watu wa namna hiyo kuweka Kanisa katika utaratibu kwa ajili ya Bibi-arusi Wake. Ajabu hiyo, sivyo? Inaonekana kama, angalao, Yeye angechukua mtu aliyefundishwa.

<sup>160</sup> Yeye ndiye Afunzaye. Yeye Ndiye anayefanya hilo. Ni ajabu kwamba Yeye amelitenda jambo hilo. Badala ya kuchukua watu wa kanisa, Yeye alichukua wavuvi kulitenda hilo. Jambo geni sana, bali ndivyo Yeye anavyotenda. Ni kweli. Ni kitendawili kwelikweli.

<sup>161</sup> Mungu alipochukua kundi la wajinga, kama tungeliwaita leo, "watakatifu wanaojifingirisha," maskini, wa mali ya ulimwengu huu, na kuwamwagia Roho Mtakatifu juu yao, kwenye chumba cha juu, badala ya kumwaga kwa Baraza la Wazee, ambako waliketi wanatheolojia wote, waliko watu wote wakuu, aliko mkuu wa makanisa yote, waliko wale waliohitimu katika Maandiko, nao wameunda shule kuu, wamefunzwa vizuri, na wanangojea kuja kwa Masihi, wanajua kwamba wao ndio watatoka waende kumpokea Yeye, na kusema, "Masihi, Wewe umeshuka kana kwamba kwenye mbawa za eropleni, Wewe umeketi chini hapa kwenye vipandio vya hekalu, tulikuona Wewe ukishuka kutoka Mbinguni, toka kwenye ukumbi wa dhahabu wa Mbinguni. Sasa sote tumefunzwa na tuko tayari kuingia kazini. Tumeelimishwa shuleni, tuna Shahada ya Sanaa, tuna Ph.D., LL.D. zetu, na yote *haya*. Sote tumefunzwa. Sisi hapa tumesimama, watu waliotimu elfu kumi. Sisi Tuko tayari kwa ajili Yako. Njoo! Tunangojea, tukiita, 'Njoo!'"

<sup>162</sup> Bali badala ya hilo, Yeye anashuka na kuchukua kundi la watu ambao ilikuwa vigumu kwao kujua tofauti ya mkono wa kulia na wa kushoto. Hiyo ni kweli. Na kuwaweka orofani, akamwaga Roho Wake, Ee Mungu, juu ya kundi la watu kama hao. Badala ya kuchukua Baraza la Wazee, Yeye alichukua wavuvi. Je, si ni ajabu kwamba Yeye hakutumia elimu yao? Ilimpendeza Mungu.

<sup>163</sup> Inaonekana inampendeza Mungu kulifanya Kanisa Lake kitendawili. Jambo lile lile Yeye analotenda hivi sasa, akifanyiza kitendawili kwa Kanisa Lake, akipita fahari zote za kipuuzi, na ghasia hii yote inayodhaniwa kuwa kanisa. Naye ata...ye yote yule ambaye Yeye anaweza kumweka mkononi Mwake, watu ambao watafungua macho yao na kuona iliyo Kweli, na kulijaribu kwa Neno la Mungu katika wakati tunaoishi, na

kuwaweka katika ule Mwili. Kitendawili! Mungu huchagua watu kama hao. Hulifanya Kanisa Lake kitendawili, watu wa kigeni, watu wa wasioeleweka.

<sup>164</sup> Wote hawa juu huko orofani, wakatoka nje wakinena kwa lugha nyingine, wakiopesuka kama watu walevi, wakiopesuka na kufanya makelele. Wanawake, mama Yake Mwe—Mwenyewe na wote hao orofani, walitoka mle, wakitatarika maneno ambayo hakuna mtu angeweza kufahamu walichokuwa wakifanya, hapo kwanza. Walikaliwa na ndimi zilizogawanyikana. *Zilizogawanyikana* linamaanisha “zilizotenganishwa.” Hakuna mtu aliyeelewa ambalo walikuwa wakifanya. Walikuwa wakipayukapayuka pale, na kutenda kama waliolewa.

<sup>165</sup> Na hapo palisimama kundi la watu waliofunzwa, wanachuoni wa Injili, wanatheologia, bali Mungu alichagua (Mungu) kuchukua na kuwaacha wadumu katika ujinga wao, wakiwa na elimu zao nyingi za juu, akaja hapa na kulitwaa kundi hili la jamaa ambao hawakujua ABC zao, naye akawamwagia Roho Wake, akabuni kitendawili kwao. Ndiyo, Mungu hutenda hilo, Yeye hutenda hilo kwa kusudi Lake Mwenyewe. Yeye hulifanya Kanisa Lake kitendawili. Ninaviamini. Ninaliamini!

<sup>166</sup> Kwa hiyo anisaidie, Mungu, ninaamini Neno! “Acha neno la kila mtu liwe uwongo, na Hili liwe Kweli.” Kile ambacho Neno hili husema kifanywe, hebu na tukitende jinsi Neno hili lisemavyo kifanywe; haidhuru linaonekana la kigeni jinsi gani, na jinsi gani unaonekana mtu wa kuchekesha, au cho chote kile. Kaa na Neno. Unaitwa mtindo wa kale, na uitwe *hili*, *lile*, au *lile lingine*, unajali nini hata hivyo? Kaa na Neno hili! Hili Ndilo, ile Kweli. Usichukue ambalo mtu mwingine anasema. Chukua ambalo Neno limesema.

<sup>167</sup> Hapa wakati fulani uliopita, rafiki yangu mhudumu... Mimi nilisikia tu hili likizungumzwa nikaliamini. Alasiri moja yenye joto kali huko chini Georgia, alikuwa anamzuru mwuza madawa. Yule mzee muuza madawa alikuwa maskini ndugu mzuri Mkristo, amejaa Roho wa Mungu. Naye akasema, “Ingia ndani ukaketi tupate kunywa ko—koka kola.” Walikuwa wameketi pale, wakinywa koka kola. Akasema, “Nataka kukuambia jambo fulani, na pengine hutaamini hili.”

“Vema, hebu tulisikie, kwanza,” akasema yule mhudumu.

<sup>168</sup> Akasema, “Nimejaribu sikuzote kumtendea Mungu kazi vizuri sana.” Yeye alikuwa shemasi katika kanisa. Akasema, “Sikuzote nimejaribu kuishi kulingana na wito wangu, na kufanya yaliyo kweli.” Akasema, “Sijamdanganya mtu ye yote. Sikuzote nimemshuhudia Bwana wangu, kila mahali nilipoweza.” Naye akasema, “Nime . . .” Akasema, “Dawa zangu hapa,” kasema, “nimejaribu kuchukua za hali ya juu sana ambazo zingeweza kununuliwa. Sijawahi kamwe kumlangua mtu ye yote. Nimejaribu kufanya kila kitu kilicho sahihi,

ambacho nilijua jinsi ya kutenda, kumtumikia Bwana.” Yeye alisema, “Nitakwambia kilichotukia.”

<sup>169</sup> Akasema, “Mwanangu, ambaye anasomea uuzaji wa madawa, pia, kunifuata, alikuwa mbele ya jengo pale siku moja.” Akasema, “Ilikuwa wakati wa kuanguka kwa uchumi.” Kasema, “Maskini bibi mmoja aliingia m—mlangoni,” akasema, “ungeweza kuona tatizo lake lilikuwa ni nini. Naye alikuwa mja mzito. Na mumewe, na wote wawili, wamevalia kimaskini.” Kasema, “Alimpa mwanangu kadi yenye maagizo ya daktari,” wakasema, “ijazwe, kwani yule mwanamke alihitaji kitu hiki ambacho daktari alimwandikia. Naye alisema, akasema, ‘Hii itakuwa kiasi kadha, kadha na kadha,’ wakati yule—yule aliyedhaniwa ndiye baba wa hiyo mimba aliuliza ‘Itakuwa kiasi gani?’ ‘Kadha na kadha.’ Akasema, ‘Bwana sitaweza kutimiza maagizo hayo, au kuijaza,’ akasema, ‘kwa sababu sina fedha kabisa.’”

<sup>170</sup> Naam, akasema, “Mwanangu alisema, ‘Shuka uende huko barabarani, umbali wa nusu jengo la mji tu, au ukipita moja la mji, geuka kushoto, nawe utaona ambako ma—mahali pale ndipo ambapo wanacho chama cha kusaidia maskini. Nawe nenda pale kwenye afisi ya wilaya, na pengine watakuwa fedha au upate hundi, kwamba watalipia maagizo haya, kwa sababu (yabidi) huyu bibi yambidi apate ile—ile—ile dawa mara moja.” Naye akasema, “Aliondoka mahali pale, akaenda zake.”

<sup>171</sup> Basi akasema yeye alimsikiliza mwanawe. “Na kitu kilisema, ‘Loo, hapana, usitende hilo.’ Kasema, ‘Huyo mwanamke anahitaji hiyo.’” Kasema, ikawa akawaza, “‘Mstari ule mrefu wa watu chini kule! Ni vigumu kwa mtu aliye mzima kusimama kwenye mstari ule, licha ya mama aliye katika hali ile.’”

<sup>172</sup> Kasema, “Nikamwambia mwanangu, ‘Nenda, waite, waambie warudi.’” Akasema, “Nami nikaenda haraka mlangoni, na kusema, ‘Rudini! Rudini!’ Wakarudi. Basi nikamwambia mwanangu, ‘Jaza hiyo. Hakuna malipo.’”

<sup>173</sup> Naye akasema, “Mwanangu alinipa ile kadi, nami nikaenda nikaijaza, na nilijaza vizuri nilivyoweza. Na nikaileta nimpe yule bibi, na kumwambia kwamba, ‘Hii haitagharimu kitu. Hilo ni sawa, sababu alikuwa akihitaji sana, na—na yasingenitatiza, kwa hiyo, malipo yake.’”

<sup>174</sup> Kwa hiyo kasema, “Nikaanza tu kuweka ile dawa mkononi mwa yule bibi. Na, nilipomwekea, nilivangalia ule mkono, nao ulikuwa una kovu.” Kasema, “Nikainua macho yangu, na nilikuwa ninaiweka kwenye mkono wa Yesu.” Kasema, “Nilijifunza wakati huo, kwamba Maandiko, yanavyomaanisha, ‘Kadiri mlivyowatendea walio wadogo kati ya hawa, watoto Wangu.’”

<sup>175</sup> Kasema, “‘Unaamini hilo?’ jamaa huyu aliniambia. Mbona, hakika, ninaamini hilo.”

Ilikuwa kitendawili, haisadikiki, bali ni kweli.

<sup>176</sup> Vipi kumhusu yule Mtakatifu mashuhuri Martin, wa Tours, Ufaransa. Wakati yeye, akiwa askari, usiku mmoja akishuka akapitia barabara yenye baridi na giza, na huko kulikuwa na... Katika barabara hii yenye baridi, na giza, alilala lofa mzee, amelala barabarani, ameganda kwa baridi. Damu yake ilikuwa inaganda kwenye mishipa yake. Naye Martin, si Mkristo bado. Na mtu ye yote ambaye amesoma historia ya Biblia, anamjua Mtakatifu Martin. Mwana historia ambaye hivi majuzi alikuwa anajaribu kuchukua kadi yake, huyo ndiye niliyemchagua kwa ule—kwa ule wakati wa tatu wa kanisa, Mtakatifu Martin, kwa sababu ishara zilifuatana naye. Basi Mtakatifu Martin akaangalia chini kabla... alikuwa askari, na hapo alikuwa amelala huyu mzee, amelala barabarani, akifa kwa baridi. Naye akatazama, na alikuwa na koti moja; bila ya hilo koti, angekufa kwa baridi. Akachukua kisu chake na kukata lile koti vipande viwili, kisha akamfunika yule lofa ndani ya hilo. Akajifunika kwa kile kipande kingine, na akaenda zake.

<sup>177</sup> Usiku ule, alipofika chumbani mwake, na kuketi chini, alimsikia Mtu anaingia mle chumbani. Akatazama, huyu hapa Yesu anakuja, amevikwa kile kipande cha koti. Huo ulikuwa mwito wake katika huduma.

<sup>178</sup> Akawa mtakatifu. Alinena kwa lugha. Shule yake ilifundishwa. Aliwafundisha watu wake kwa Neno la Mungu tu. Hakujali liliyosema Kanisa la Kwanza la Rumi au lo lote kati yao liliyosema. Alidumu sawasawa na Neno la Mungu. Aliwafundisha; kunena kwa lugha, na kuwekea mikono wagonjwa. Wao walifufua wafu. Waliwatoa pepo. Mtu mmoja, rafiki yake, aliuwawa, naye alikwenda na kujinyoosha juu yake, (akaomba amwone kwa dakika chache), yeye na rafiki yake wakatoka wakitembea, pamoja. Kwa nini? Ilikuwa ni kitendawili. Hakika, Mungu alilitenda.

<sup>179</sup> Naamini katika vitendawili. Ndiyo, bwana. Ninaamini. Ninaviamini, kwa moyo wangu wote.

<sup>180</sup> Ilikuwa ni kitendawili wakati, kati ya watu wote wenye akili waliokuwepo ulimwenguni, Mungu aliweka ufunguo wa Ufalme mikononi mwa mtu aliyefikiriwa “asiye na elimu wala maarifa.” Hilo ni kweli. Mmoja wa watu hodari sana ulimwenguni, katika siku ile, alikuwa ni Kayafa, kuhani mkuu, wengine walikuwa ni watawala wa madola na wafalme, na watu wakuu wa dunia, kama marais na kadhalika, watu hawa wote walio wakuu.

<sup>181</sup> Na ni kitu gani muhimu kuliko vyote ulimwenguni? Ni Kanisa la Mungu! Mungu aliumba dunia, Yeye aliumba kwa kusudi fulani: kutoa Kanisa kutoka humo, Bibi-arusi. Na hiyo ndiyo kazi iliyokuwa muhimu sana ulimwenguni.

<sup>182</sup> Na watu hodari kuliko wote aliokuwa nao Yeye ni watawala wa madola na wafalme, na watu wenye mamlaka na masultani,

makuhani wakuu na watu wa kanisa. Angeweza kuchukua ye yote wa hao. Bali ilikuwa ni kitendawili hapo Yeye alipoita mtu ambaye hakuweza hata kuandika jina lake mwenyewe, akasema, “Nitakupa wewe funguo za Ufalme. Lo lote unalofunga duniani, Mimi nitalifunga Mbinguni. Lo lote unalolifunga duniani, Mimi nitalifunga Mbinguni.”

<sup>183</sup> Aisee, nimefikiria tu jambo hilo kuhusu lile ono, “Cho chote unachofunga au unachofunga.”

<sup>184</sup> “Cho chote unachofunga duniani, nitakifunga Mbinguni. Cho chote unachofunga duniani, nitakifunga Mbinguni.” Ndiyo, Yeye alitoa hilo si kwa yule kuhani mkuu mwenye elimu, Kayafa, bali kwa mvuvi asiyejua kitu. Kweli ni kitendawili!

<sup>185</sup> Tunamwona Paulo, maskini Myahudi mwenye pua lililopindika, akienda zake, mwenye kiburi, akishuka kwenda kuwafunga hao watu wanaofanya makelele, na kupaza sauti na kadhalika; akiwatupa gereza, akiliangamiza Kanisa; wakampiga mawe Stefano, akashuhudia jambo hilo, na akishikilia makoti yao. Yeye—yeye alikuwa tisho. Mungu angehagauje mtu kama huyo?

<sup>186</sup> Na, angalia, maaskofu, mitume wote, walisema, “Tutafanya uchaguzi, mtu fulani wa kuchukua mahali pa Yuda.” Basi walimchagua nani? Walimchagua Mathiya. Mathiya, ninaamini ndilo jina lake. Mathiya, ndiyo. Mathiya, walimchagua kwa kupiga kura, na hakuna kitu hata kimoja alichowahi kufanya. Alielekea kuwa mtu mwenye haki. Naye Mungu akamchagua mtu mwenye hasira kuliko wote, mbaya kuliko wote nchini, kuchukua mahali pake. Kitendawili. Hilo ndilo ambalo Mungu hufanya. Kitendawili!

<sup>187</sup> Ilikuwa kitendawili wakati huyu Myahudi asiyempenda Mungu, mwenye majivuno, mwenye hasira kali, mchoyo, aliyedharauliwa, alikuwa akishuka akienda zake, siku moja, kuelekea mjini, kuwakamata Wakristo na kuwafunga jela, na hapo, mara tu, alipigwa akaangushwa chini. Naye alipotazama juu, hapo ilisimama ile Nguzo ya Moto, na Sauti inakuja, ikisema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi Mimi?” Ilikuwa kitendawili alipoweza kuiona Hiyo, na wengine wote hawakuweza kuiona Hiyo. Unaona?

<sup>188</sup> Mtu fulani alisema, “Loo, siioni Hiyo kamwe. Hakuna kitu kama hicho hapo; ndiyo, huioni. Hilo ni kosa.” Kuhusu hili leo hii, wanasema hivi, “Siamini hilo.” La, hakika la. Kwa kweli huwezi. Bali kuna hao hapo, wao hapo ambao wanaiona Hiyo. Hakika, kama huwezi, wewe u kipofu, huwezi kuiona Hiyo.

<sup>189</sup> Jamaa mmoja aliniambia, wakati fulani uliopita, ilikuwa miaka kadha iliyopita, akasema, “Sasa, kama ninakuudhi...” Akasema, “Naam, Paulo alimpiga mtu kwa upofu.” Akasema, “Kama mimi ni wa ibilisi,” akasema, “nipige kwa upofu.”

<sup>190</sup> Nikasema, “Hilo si lazima lifanywe. Tayari u kipofu. Unaona, tayari u kipofu. Wewe ni kipofu wa aina mbaya kuliko zote, unaona.” Nikasema, “Ana, hekaluni, aliweza kuona mbali zaidi kuliko unavyoweza kuona. Naye alikuwa kipofu, kimwili.” Yeye alikuwa kipofu, kiroho. Hakika. Ilikuwa kitendawili.

<sup>191</sup> Ilikuwa kitendawili wakati Mungu aliposababisha kilichodhaniwa ni uzushi... Makelele yote haya, na kupaza sauti, na kumsifu Mungu, na kunena kwa lugha, na watu ambao wanadharauliwa na kukataliwa, na kuitwa baradhuli na wazushi; ni kitendawili wakati Mungu, Baba mkuu wa wote, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Ambaye alichagua kundi la “wazushi” kuleta wokovu kwa Kanisa Lake, badala ya taratibu ya kidini, na ya kitheolojia iliyofundisha vizuri. Ni kitendawili.

<sup>192</sup> Si muda mrefu uliopita nilikuwa kwenye mji fulani huko Washington, au, la, naamini ilikuwa Oregon. Na hapo alikuwepo—alikuja mwandishi wa habari, waandishi wadogo wawili wa habari, walikuwa na sigara mkononi. Wakaja. Walikuwa wanataka kuandika habari zangu, naam, hakika, vizuri sana, unajua. Nao walikuwa wakiendelea, wakisema jambo hili na jingine. Naye alisema, “Na, wewe u mtakatifu anayefingirika?”

<sup>193</sup> Nikasema, “La.” Nikasema, “Sijafingirika kamwe. Bali,” nikasema, “na—nadhani kama Yeye angeniambia nijifingirishe, ningejifingirisha.”

<sup>194</sup> Na hivyo akaendelea kuzungumza namna hiyo, unajua. Naye alikuwa akiendelea, akasema, loo, akiendelea. Nikasema, “Hebu tu nikuambie jambo fulani, bibi mdogo, andika cho chote unachotaka kuandika. Wewe u Mkatoliki.”

<sup>195</sup> Akasema, “Hilo ni kweli.” Akasema, “Ulijuaje nilikuwa Mkatoliki?”

<sup>196</sup> Nikasema, “Naam, jinsi ile ile ninavyojua yale mambo mengine kule jukwaani, unaona.” Nikasema, “Wewe u Mkatoliki. Basi nenda ukayaandike, bali ninakuonya sasa hivi; mnamo siku thelathini tangu sasa, yaandike, na utakuwa umelala kando ya barabara, huku koo lako limekatwa na kioo cha gari lako, ukilia kwa sauti kuu upate rehema, nawe utawaza juu yangu mara nyingi.”

Akasema, “Wewe si Muairishi?”

“Ndiyo.”

“Watu wa kwenu walikuwa Wakatoliki?”

Nikasema, “Labda walionitangulia.”

<sup>197</sup> Akasema, “Mama yako angefikiria nini kuhusu jambo hilo, kuhusu wewe kufanya jinsi...”

<sup>198</sup> Nikasema, “Nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo. Na akampokea Roho Mtakatifu. A-haa. Ndiyo.”

<sup>199</sup> Kisha nikasema, “Sasa, kama unataka kuendelea namna hiyo, basi nitachukua jina lako na wewe uchukue jina langu. Basi kama halitatumia basi, baada ya siku thelathini, wewe liandike kwenye gazeti kwamba mimi ni nabii wa uwongo. Basi ondoka ukayaandike.”

<sup>200</sup> Akasema, “Naam, ningechukua kufikiria, wakati nitakapofika Mbinguni, kwamba kundi la baradhuli, kama lililo juu kule kwenye mkutano ule, litakuwa linatawala Mbinguni.”

<sup>201</sup> Nikasema, “Hutakuwa na shida sana.” Nikasema, “Sidhani, mimi sidhani... Isipokuwa ubadilishe nia yako na njia yako, hutakuwepo Huko, kwa vyo vyote, unaona.” Nikasema, “Kwa sababu, watakuwepo Huko. Mungu amewachagua hao.”

<sup>202</sup> Ni kitendawili, kwamba Mungu amechukua wapumbavu, unaona, mambo hayo. Yeye, Mungu, alichagua kuleta wokovu ulimwenguni kupitia kundi kama hilo, kitendawili, tofauti kabisa na wanachuoni wao waliopata mafunzo ya juu sana na walioadibishwa kwelikweli, na wathelolija na kadhalika. Mungu huwaacha hao. Huchukua maskini baradhuli fulani hivi na kumwinua, na kuweka Ujumbe Wake ndani yake, kama alivyomfanya Yohana, baadhi ya hao wengine, Petro na wengineo, akawatuma na kuhubiri Injili, na kuleta Kanisa Lake; na kuwaokoa, na kuwaleta tena duniani, na hakuna zaidi ya hayo, unaona. Na kuachilia upuzi huu wote mkuu wa kielimu uondoke. Loo, jamani, ajabu hiyo bila shaka! Ninge... .

<sup>203</sup> Mungu, wakati Mungu alipochagua wasio na elimu na wasio na maarifa, badala ya walioelimika na wenye maarifa, kuwa Bibi-arusi Wake! Hivi ungeweza kuwazia mtu, akichagua bibi-arusi wake, angechukua... .mtu mkuu sana, mwenye mamlaka ya juu sana.

<sup>204</sup> Ninalo jambo dogo hapa nililotaka kusema, bali sitapata muda wa kulisema, kuhusu mfano mdogo nilioona wakati mmoja. Bali sitaweza kuusimulia. Nilivandika chini hapa, lakini sina muda wake.

<sup>205</sup> Lakini, Mungu alimchagua Bibi-arusi Wake kutoka kwenye kundi la watu kama hao. Naam, mtu awaye yote anayesema kwamba hivyo siyo ilivyo, basi huamini Biblia yako. Hilo ni sawa kabisa. Soma Biblia yako, hivyo ndivyo ilivyo hasa.

<sup>206</sup> Ilikuwa ni kitendawili hasa wakati Mungu alipochagua upumbavu wa mahubiri yenye uvuvio badala ya theolojia motomoto. Mtu ambaye hajui, kwa shida, hutumia “iki, aiko, tote, jukua, pepa,” maneno yote kama hayo, na—na kusema kila namna ya—ya mambo nje ya sarufi yake, na hayana ufasaha wa lugha, na mambo chungu nzima hivyo. Basi Mungu alichagua hao badala ya kuchukua wanachuoni waungwana, ambao wanaweza kweli kutamka maneno na kuyasema sawasawa. Bali ilimpendeza Mungu kuchukua upumbavu wa mahubiri yaliyo na uvuvio, mkulima mdogo fulani asiyejua ABC zake, na

kumchukua mtu yule na kuwaokoa watu kwa yeye. Ambapo, wadanganyifu, wote wameadibishwa, wakiwaongoza tu, kipofu akimwongoza kipofu mwenzake. Kitendawili kwelikweli.

<sup>207</sup> Loo, Neno limejaa mambo hayo sana. Masomo mengi hapa, au vifungu, inanibidi ku—kuyaacha.

<sup>208</sup> Ni kweli kwamba kanisa kuu linang'aa na kumetameta, kwa theolojia motomoto, ambapo Ufalme humeka kwa unyenyekevu, maskini na wanyenyekevu. Injili haing'ai, inameka. Dhahabu ya uwongo hung'aa; dhahabu halisi humeka. Ipo tofauti kati ya kumeka na kung'aa. Tunajua hilo. Ambapo kanisa kuu humetameta na kung'aa kwa wanachuoni waungwana sana, viti vizuri kanisani, msalaba wenye sanamu kila mahali ukutani, na miundo na majengo ya hali ya juu sana, na vitu vyenye minara mirefu, yote namna hiyo; Ufalme ule mdogo, chini kwenye kitu kama kichochoro fulani kidogo hapa, mahali fulani, unameka kwa Utukufu wa Mungu, umejazwa na walio wanyenyekevu wa mioyo, unaona, Mungu akitenda kazi ndani yao, akiwaponya wagonjwa, na akifufua wafu, na kutoa pepo, na kadhalika namna hiyo; anawaachilia tu wapite.

<sup>209</sup> Palikuwa na mkutano wa wahudumu. Usilisahau hili. Palikuwa na mkutano mkubwa wa wahudumu hapa hivi majuzi, katika mji fulani, ambapo baadhi ya watu kutoka papa hapa walikuwepo penye mkutano ule. Na walikuwa na mtu fulani ambaye alikuwa akienda ku-... Loo, yeye alikuwa mwanatheolojia, "alikuwa na ujumbe wa wakati huo, kwa ajili ya watu." Naye alikuwa ameusomea kwa majuma mawili au matatu. Hilo lilikuwa sawa. Basi alipokwenda jukwaani, hakuna hata mkunjo kwenye nguo zake, jamani, amevaa nadhifu kabisa, wajua, akaenda kule juu na akabenua kifua chake na kuweka vyote—vitu vyake vya huo ujumbe wake. Naye kweli akahubiri hasa ujumbe wa saa moja ambao haungeguswa, kiakili. Loo, jinsi alivyobenua kifua chake, na kuchukua jina la Daktari LL *Fulani*, toka shule fulani kubwa. Huo ulikuwa wa kiungwana sana na wa kielimu, hata akawaletea watu kipeo kikubwa sana, cha saikolojia na kadhalika. Akasema, "Ulikuwa mzuri kwelikweli."

<sup>210</sup> Bali Wakristo wakiketi pale, kama tu kwenye Baraza la Nikea, ilimhuzunisha tu Roho. Loo, ulikuwa kipeo, hakika. Ndiyo, bwana. Ulikuwa wa hali ya juu sana, jinsi ilivyowezekana. Bali wale watu waliojawa hasa na Roho, ilikuwa tu, "Ha?" Haukufua dafu... Hapakuwa na Roho pale kuunga mkono.

<sup>211</sup> Kwa hiyo aliposhuka, aliinamisha kichwa chake chini, aliona haukukolea sawasawa. Alitoka kwenye shule nyingine; naye alikuwa na wapentekoste. Kwa hiyo aliposhuka kwenye jukwaa, manyoya yake yameinama. Akaanza kutembea akielekea kule, na vitu vyake chini ya kwapa lake, *hivi*, akipita katikati ya kusanyiko.

<sup>212</sup> Kulikuwa na mzee mtakatifu mwenye hekima upande wa kulia, akamsogelea mtu mwingine, akasema, “Kama angelipanda juu jinsi alivyoshuka, angeshuka jinsi alivyopanda juu.” Ndivyo ilivyo. Kama angelipanda kwa unyenyekevu, labda angelishuka amejawa na Utukufu. Kama angelipanda juu namna ile alivyoshuka chini, angeshuka jinsi ile alivyopanda juu. Hiyo ni kweli. Kitendawili!

<sup>213</sup> Sikilizeni, katika kufunga sasa, kwa muda mfupi sana kabla ya mstari wa maombi. Nataka kusema neno jingine, kama mawili, kuhusu kitendawili.

<sup>214</sup> Maono ya manabii wa kale bado ni kitendawili. Hayaguswi. Nani awezaye kusema kwamba mtu, miaka elfu nne iliyopita, angeweza kuzungumza kuhusu magari yasiyovutwa na farasi yakisongamana kwenye njia pana, yenyewe kwa yenyewe. Wale manabii wa Agano la Kale, jinsi walivyotangulia kuona mambo na kuyatabiri, waliinuliwa kwa Uweza wa Mungu, ambapo waliona jambo hilo kule mbali kwenye miaka ijayo, na wakalitabiri kwa usahihi mkamilifu. Hebu lieleeze! Ni kitendawili. Loo!

<sup>215</sup> Kingine, nataka niwape kimoja kidogo, kisicho na maana. Bali, kuongoka kwangu kulikuwa kitendawili. Nanena hili kwa upendo na heshima. Wazazi wangu wameaga dunia. Jamii yote ya mama yangu walikuwa wenye dhambi, wategaji wa wanyama, wawindaji, na watu wa milimani. Jamii yote ya baba yangu walikuwa walevi, wauza chang’aa, wacheza kamari, wapiga bunduki, wakiuana, wengi wao walikufa kiume. Hapakuwa na chembe ya dini, kwa namna yo yote, kwetu. Vipi basi Mungu. . . ilikuwa ni nini Kile ambacho kilikuja kwenye kile kibanda kidogo kilichochakaa juu kule asubuhi ile, kile mnachoonna katika picha kwenye ukuta ule? Nini? Ni tofauti kabisa.

<sup>216</sup> Kama ukipanda chembe ya ngano ardhini, itazaa chembe ya ngano. Ukipanda mahindi ardhini, yatazaa mahindi. Ukipanda gugu ardhini, litazaa gugu.

<sup>217</sup> Bali hiki ni kitendawili! Kila mmoja wenu anaweza kusema jambo lilo hilo juu ya nafsi yake. Sisi sote tunaweza kufikiria kuhusu kitendawili cha yale yaliyotukia.

<sup>218</sup> Hapa pana kitendawili kingine. Mimi ninawezaje, baada ya kuhubiri karibu miaka thelathini, bado ningeweza kuhofia wazo lile la kuvuka kwenda Ng’ambo ya Pili? Ingewezekanaje? Baada ya kuhubiri tangu nilipokuwa mvulana mdogo, na sasa hapa ni mtu wa miaka hamsini na miwili, na kisha kufikiria kuhusu kuhofia. . . si—siku. . . Nilijua nimeokoka. Bali, nilihofia hilo wazo. . . Bali upendo wa Mungu, asubuhi moja, ulishuka chumbani mwangu, ukaniinua juu, na kunichukua Mahali walipo waliokombolewa. Kitendawili kwelikweli!

<sup>219</sup> Nataka niwaulizeni jambo fulani. Naweza pengine niukatize huu hapa sasa. Nataka niwaulize jambo. Ni nini Kile kilicho

juu ya picha ile pale? Kilitoka wapi? Kipo hapa kwa ajili gani? Sayansi haiwezi kukikana Hicho. Ni Kitu gani katika mikutano, ambacho husimama pale na kuwachungua watu kabisa, na kuwaambia, “Nyuma huko, ulichotenda. Upo hapa kwa kusudi *hili*. Upo hapa kwa ajili ya *hilo*”? Haliaminiki kwa akili za kisayansi.

<sup>220</sup> Naam, tunajua uwezo wa kupitishiana mawazo. Uwezo wa kupitishiana mawazo ni, kusema jambo, kama vile unasema jambo nami ninaweza kusema jambo lile lile, unaona, au, ninayasoma mawazo yako, hilo linatukia wakati uo huo. Bali unapoona kwamba Hicho kinatamka mambo ambayo yatatukia huko mbele siku za usoni, hilo hutupilia mbali uwezo wa kupitishiana mawazo.

<sup>221</sup> Haisadikiki kwamba Mungu, katika siku hizi za mwisho, kama Yeye alivyoahidi angetenda, angetenda jambo kama hilo. Bali ni kweli, ni kitendawili! Mungu yeye yule ambaye sikuzote amekuwa na vitendawili na kuvionyesha, Yeye ni Mungu yeye yule leo, kwa sababu Yeye hushika Neno Lake. Sayansi haiwezi kukikana Hicho, Hicho hapo kwenye mitambo ya kamera. Ni kitendawili, Mungu!

<sup>222</sup> Ni Kitu gani? Katika—katika Kutoka, sura ya 13, twasoma kwamba Mungu aliwapa wana wa Israeli, ambao walikuwa mfano wa kanisa leo; walipokuwa wanasafiri katika mwili, sisi tunasafiri katika Roho. Jumapili ijayo tunalichukua hilo, sasa. Kumbuka, yote ni juu ya hilo, unaona. Sasa, jinsi ambavyo—kwamba ambapo walianguka chini, kimwili, *hivi*, na Mungu alikuwa pamoja nao; Kanisa limeketi pamoja na Kristo, katika Ulimwengu wa Roho, katika milki za kiroho, likiendelea na falme zote chini ya miguu yetu. Haleluya! Ndiyo, bwana. Nao walikuwa na Nguzo ya Moto, Nuru ambayo waliifuata. Po pote pale Nuru hii ilipokwenda, waliifuata Nuru ile. Maelfu ya miaka imepita, mamia na mamia ya miaka yamepita, na bado inaishi. Kitendawili! Yeye yule jana. . . Ikitimiza Maandiko, Ipo hapa kwa ushuhuda; si kwa sababu ya sisi, bali kwa sababu kwamba Mungu aliahidi Hiyo, kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Huo ndio Musa alihesabu, ule utajiri wa Kristo, au kushutumiwa Kwake Kristo kuwa utajiri mkuu kuliko hazina za Misri. Na Kristo aliyekwenda mbele Yake alikuwa nini? Nuru, Nguzo ya Moto.

<sup>223</sup> Alisema, “Nimetoka kwa Mungu na ninarudi kwa Mungu.” Alirudi. “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona Mimi; kwani nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Kuendelea hata mwisho wa ulimwengu, Yeye angekuwepo hapo, pia. Tumefika!

<sup>224</sup> Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Mtakatifu Paulo alikutana na Yeye njiani akienda Dameski, Yeye alikuwa amerudi kwenye ile Nguzo ya Moto.

225 Karibu miaka elfu mbili imepita tangu wakati huo, na ndiye Huyu hapa! Si miongoni mwa madhehebu, si katika kikundi cha wanachuoni walioadibishwa wa siku hizi, bali kundi la maskini na wanyenyekevu. Kitendawili! Kitendawili! Kwa wale wanaompenda Yeye, wanaomwamini Yeye, maelfu ulimwenguni ambao walimwamini Yeye, ni kutimiliza ahadi Yake ya Agano Jipya na la Kale pia. Ndivyo ilivyo. Bali ni Kitendawili!

226 Ilikuwa kitendawili wakati Mungu alipoahidi kuutoa Ufalme kwa kundi dogo, badala ya kanisa kuu lenye taratibu. “Msiogope kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa ninyi ule Ufalme.” Itakuwa . . . Ni kitendawili. Ni kitendawili.

227 Itakuwa ni kitendawili hasa, moja ya siku hizi, Yesu ajapo; nao waliokufa katika Kristo watafufuka, na huu uharibikao utavaa kutokuharibika, ndipo Kanisa litanyakuliwa.

228 Katika nyakati hizi za Krismasi, wakati watu wananunua vitu madukani, na kucheza dansi, na kunywa, na kusherehekea jambo ambalo hawajui habari zake kabisa, kana kwamba wanaadhimisha siku ya kuzaliwa kwake Washington au Lincoln, na sio kuabudu ile . . . Wao wangali wamemweka Mungu horini.

229 Ambapo, Mungu hayuko horini. Yeye amefufuka katika wafu, naye yu hai hata milele na milele, akiishi miongoni mwetu, akijithibitisha Mwenyewe, kuwa ni Mungu yeye yule ambaye walimbeba wazee wa Nikea, na katika miaka yote iliyopita amekuja tangu Siku ya Pentekoste. Mungu yeye yule aliyekutana na Paulo akienda zake Dameski; yeye alikuwa mmishenari kwa Mataifa, na mjumbe toka kwa Mungu, kwa Mataifa. Ujumbe wa Mataifa ulianza kwa kuzuriwa na Nguzo ya Moto, na unaishia jinsi ile ile.

230 Ufalme wa Mataifa ulianza, ufalme wa ulimwengu, huo ni ulimwengu, ulianza na kukemewa kwa lugha ya Kimbinguni, katika siku ya mfalme Nebukadreja; unakwisha kwa kitu kile kile, Roho Mtakatifu alipomwagwa juu ya kanisa la Mataifa, la siku ya mwisho, kukemea nchi za Mataifa tena kwa maandiko ukutani. Maandiko ukutani, kwamba, Mungu tayari ameandaa Kanisa Lake, Yeye ameandaa watu Wake, Yeye ameandaa mahali Pake, nao wanamngojea Yeye aje.

231 Na kule kunyakuliwa! “Tarumbeta ya Mungu itakapolia, nao waliokufa katika Kristo watakapofufuka, sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa maana tarumbeta ya Mungu italia, waliokufa katika Kristo watafufuka; nasi tutanyakuliwa pamoja nao, ili tumlaki Bwana hewani.” Kitendawili, moja ya asubuhi hizi, wakati makaburi yatakapofunuka nao wafu wanatoka; wakati wale walio hai watabadilishwa, mara moja, kufumba na kufumbua, na kutwaliwa hewani kumlaki Yeye.

232 Jambo lote ni kitendawili, Mungu akitenda kazi miongoni mwa watu Wake. Mnaamini hilo? [Kusanyinko linasema, “Amina!”—Mh.] Tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi mafupi.

233 Ee Mungu, sasa kwa zaidi ya saa nzima, na yapata saa moja na dakika kumi, tumesimama hapa tukizungumzia kuhusu matukio yaliyopita na ya sasa, jinsi Roho Mtakatifu anavyoyagawanya, Bwana, kama Neno la Mungu lilivyokwishafanya kwa neema, kuonyesha kwamba yule Mungu hasa wa Mbinguni, Yule aliyeishi katika siku za kale, katika umbo lile lile na namna ile ile, Yu hai leo. Maajabu yale yale, na Uweza ule ule ambao ulikuwa juu ya manabii wa kale, ambao ulikuwa juu ya Kanisa hapo Pentekoste, ulikuwa juu ya Hana; na juu ya Agabo, manabii wa Agano Jipya katika zamani zile, ambaye hata alimsahihisha Mtakatifu Paulo. Na Mtakatifu Paulo akaingia kwenye matatizo kwa kutokumsikiliza Agabo, sababu Agabo... Ingawa yeye alikuwa mtume, Paulo alikuwa mtume, bali Agabo alikuwa na Neno la Bwana, naye akamuonya asiende kule. Bali Paulo alikusudia kwenda, ndiposa akapata matatizo. Basi, Baba, sikuzote tunapata matatizo kama hatutii Neno la Mungu.

234 Nasi tunaona kwamba Mungu yeye yule ambaye alikuwa pamoja na wale ndugu kule, ndiye Mungu yeye yule leo hii. Tunamwona Yeye katika kila udhihirisho. Na jambo hilo ni kitendawili, Bwana. Ulimwengu unaangalia, na hutikisa vichwa vyao, na husema, “Hilo si kitu.” Mwamini analikubali Hilo na hulikumbatia, na anajua kwamba Hilo ni Mungu aliye hai.

235 Ee Baba, tunaomba asubuhi hii, kwamba kama kuna mtu fulani miongoni mwetu ambaye hajawa mwamini bado, kwamba hii itakuwa saa yao ya kuamini. Ee Mungu, jalia hilo sasa hivi tu katika moyo wa kila mtu ambaye yuko hapa, ambaye hamjui Kristo kama Mwokozi wake, kwamba hii itakuwa saa ambapo patakuwa na kitendawili mbele yao; kwamba maskini mwenye dhambi mchafu (asili yake ni mwenye dhambi, amezaliwa ulimwenguni katika dhambi, ameumbwa katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uwongo, kwa uchafu) angeweza kubadilishwa na kuumbwa katika haki ya Mwana wa Mungu. Jalia, Bwana, kwamba, kwamba hicho kitendawili kikubwa kitafanyika katika mioyo ya wote hapa asubuhi hii ambao hawakujui Wewe kama Mwokozi wao na Mfalme wao ajaye, na wako tayari kukulaki Wewe katika tarumbeta ya mwisho kama ingelia leo.

236 Ndipo tutaomba pia, Bwana, kwamba Wewe ungewakumbuka wale hapa ambao ni wagonjwa na wanaoteseka. Ee Mungu, leo tunaomba kwamba Wewe utamponya kila mtu ambaye ni mgonjwa au anateseka. Hebu wajue kwamba Mungu yungali anafanya vitendawili kwa mtu ye yote ambaye atatimiza Neno Lake.

<sup>237</sup> Twajua Neno Lake ni kitendawili. Wakati Hilo linapoahidi jambo lisilo la kawaida kabisa, kwa ulimwengu, jambo ambalo hawawezi kulielezea, ni—ni jambo lipitalo ujuzi wao na—na ufahamu. Bali wakati moyo mnyofu utalichukua Neno lile na kulizamisha Hilo katika vina vya utu wao, ndipo Neno hilo huzaa kweli zilizo hai za ile ahadi.

<sup>238</sup> Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya hili, kwamba kuna watu wanyofu ambao wanaamini Ujumbe huu. Hatutazamii ufalme ambapo enzi za atomiki zitatawala, bali tunatazimia Ufalme ambao Kristo atatawala katika uweza na utukufu, wa amani na utukufu, juu ya dunia; si ambapo tutabonyeza miguu yetu kwenye gari, pedeli za petroli, au kuruka angani kwa ndege aina za jet; bali ambapo tutaketi kukizunguka Kiti cha Enzi cha Mungu aliye hai, loo, na kumwangua Yeye, na kumwona Yeye aliyejeruhiwa kwa makosa yetu na kuchubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na Ambaye kwa mapigo Yake tumepona. Hamu ya mioyo yetu, Bwana, tangu kile kitendawili kikuu kilipokuja juu yetu, ni kwamba tutafika Kwake na kuketi pamoja na Yeye siku ile. Tujalie hilo, Bwana. Twaomba hili katika Jina la Yesu.

<sup>239</sup> Huku tumeinamisha vichwa vyetu. Nauliza, katika mkutano huu asubuhi hii, iwapo mtu ye yote angetaka kukumbukwa katika maombi, na aseme, “Bwana Mungu, ninauinua mkono wangu Kwako”? “Na, Ndugu Branham, utaangalia na kuona mkono wangu, na kuniombea, kwamba kitendawili kikuu kitatendeka moyoni mwangu, hata nitakutana na Kristo katika ubatizo wa Roho na Uweza wa kufufuka Kwake.” Mungu awabariki, kila mtu, na kila mmoja. Hilo ni sawa. “Kwamba nitakutana na Mungu.” Na Mungu awe pamoja nanyi. “Nitakutana na Yeye, na kitendawili kikuu kitatukia maishani mwangu, nami nitajazwa kwa uwezo Wake na utukufu Wake, na wema na rehema Yake Yeye aliye hai milele na milele. Na siku moja nitahesabiwa katika kitendawili kinachokuja. Kitu ambacho wakati...”

<sup>240</sup> Vumbi la manabii wale linakaa kule ardhini. Hapo vumbi la mashahidi wale ambao waliliwa na simba, wakasambazwa pamoja na kinyesi cha simba mavumbini, na kila mahali duniani, hata hivyo Kristo ataufufua huo mwili tena! Inaonyesha kwamba Yeye ni ufufuo.

<sup>241</sup> Wakati Yeye alipochukua matope kidogo kutoka kwenye mikono Yake na kuyaweka kwenye macho ya mtu ambaye hakuwa na macho kamwe, ilionyesha kwamba binadamu alifanywa toka vumbi la ardhi, naye akarudi akiwa ana mboni za macho na angemwona Muumba ambaye alimuumba.

<sup>242</sup> Kama Mungu hokusudii kufufua wafu, basi kwa nini Yeye alifanyika mwili kama sisi, na kurudi kuelekea kwenye

mavumbi, na kujifufua Mwenyewe tena? Kwa nini Yeye alijifufua Mwenyewe iwapo hakuna ufufuo wa wafu? Loo, hebu tusiwe watoto, bali hebu tuwe wanaume na wanawake katika Roho, tumwamini Mungu kwa mioyo yetu yote.

<sup>243</sup> Kungekuwepo na mwingine sasa, kabla hatujaanza kuomba? Mungu akubariki, na wewe, ndugu yangu, na wewe. Ndiyo.

<sup>244</sup> Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunakuletea Wewe hawa ambao wameinua mikono yao. Kwa namna fulani au nyingine, Roho Mtakatifu amefanya njia Yake katika mioyo yao, hapo akiwaambia, “Hampo hapa kwa ajili ya kula na kunywa, na—na kulala, na kuamka mwende kazini; halafu mkarudi, mkala na mkanywa na kulala tena. Mpo hapa kuwa wana na mabinti wa Mungu. Mpo hapa kuchukua nafasi na mahali penu katika Kristo. Na Mimi nipo hapa asubuhi hii kuwaita,” angenena Roho Mtakatifu kwa maisha yao.

<sup>245</sup> Baba, kwa maombi, silaha pekee ambayo ninajua, nawakabidhi Kwako. Basi ni—ninampinga adui ambaye angewazuia wasije Kwako. Naweka, kwa imani, Damu ya Yesu Kristo kati ya adui na wao, ambaye angewatenga na tukio hili tukufu la kitendawili hiki kikubwa, cha kumpokea Roho Mtakatifu na kupata Uzima wa Milele. Kwani tunatambua hilo ndilo jambo pe—pekee lililopo, suluhisho pekee ambalo tumepewa, kwa ajili ya Uzima wa Milele, ni kuwa na Uzima wa Mungu ndani yetu, hapo inakuwa Uzima wa Milele ndani yetu. Likirimie, Bwana, kwamba litatukia kwa kila mmoja aliyenyosha mkono wake. Na labda wale ambao hawakuwa na ujasiri wa kuinua mikono yao, wakirimie hilo, pia. Sasa, Baba, ni Wako. Nawatoa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

<sup>246</sup> Na sasa wakati mstari wa maombi utaundwa, Baba, sijui nani atakayekuja juu hapa. Bali tupe kitendawili kingine asubuhi hii, Bwana. Jalia Uweza mkuu wa ajabu wa Mungu ushuke chini na ufanye jambo fulani kama Wewe ulivyoahidi. Na hii itakuwa mara yangu ya kwanza, Bwana, tangu kukutana na Wewe juzijuzi. Naomba sasa kwamba utayajibu maombi ya watu, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>247</sup> Sasa ningefurahia kama kila mmoja angeketi tu, mkiweza, kwa muda kidogo tu.

<sup>248</sup> Sasa, mtu ye yote ambaye ana kadi ya maombi. Billy alishuka akaja asubuhi hii, kama alivyoahidi angefanya, naye akatoa kadi za maombi kwa baadhi ya watu hapa. Alisema hapakuwepo na wengi sana. Tafadhali inueni mikono yenu, wale ambao wana kadi za maombi. Sawa. Naomba kama mngechukua mahali penu tu na kusimama hapa mstarini, wale ambao wana kadi za maombi. Yuko wapi, Billy, uko wapi? Loo, sawa. Hebu simameni tu hapa mstarini.

<sup>249</sup> Naam, kila mmoja na aombe sasa. Tunakuja mbele za Bwana Mungu wetu. Sasa hebu na tuimbe wimbo ule na muziki,

tafadhali, wakati Dada Arnold anacheza pale. Wote pamoja sasa, kwa kimya kimya.

Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu;  
Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu.

[Ndugu Branham anaanza kuugugumiza *Amini Tu*—Mh.]

... amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu;  
Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu.

<sup>250</sup> [Ndugu Branham anaanza kuugugumiza *Amini Tu*, kisha anasoma Marko 11:21-24—Mh.]

... *Petro akakumbuka habari yake akamwambia, Rabi, tazama, mtini ulioulaani umenyauka.*

... *Yesu akajibu, akamwambia, Mwamini Mungu.*

*Amini, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila amini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.*

*Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*

<sup>251</sup> Yesu alisema, wakati mmoja ambapo wao hawakuelewa kwamba Yeye alikuwa jinsi Yeye alivyokuwa, Yeye alisema, “Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi ambazo ninatenda. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi ninyi msiniamini Mimi. Bali kama nazitenda kazi za Baba Yangu, basi ninyi aminini zile kazi.”

<sup>252</sup> Nimemaliza hivi punde, asubuhi hii, kuleta Ujumbe wa—wa *Kitendawili*. Kitendawili ni jambo ambalo halina maana, bali kwa—kwa kweli halisadikiki, asema Webster, bali ni la kweli. Jambo ambalo ni vigumu kuliamini, ambalo huwezi kulielewa, ni fumbo.

<sup>253</sup> Yesu alitenda kazi za Baba Yake kwa sababu Baba alikuwa ndani Yake. Hiyo ndiyo sababu kazi zile zilitendeka, kwa sababu Baba alikuwa ndani ya Mwana. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kwamba, ndani Yake, Yeye alikuwa Mungu aliyefanyika mwili. Mnaamini hilo? [“Amina.”] Kwamba, Mungu Baba, ambaye ni Baba wa Yesu Kristo, yule Roho Mkuu alikaa (katika utimilifu wa Uweza Wake) katika Yesu Kristo, ambaye alikuwa maskani ya Mungu, aliyefanyika mwili na kukaa duniani, akiwakilisha Neno. Yesu alikuwa Neno. Biblia ilisema hivyo, Mtakatifu Yohana, sura ya 1. Na Neno lilikuwa halionekani. Sasa sikilizeni kwa makini. Neno halikuonekana mpaka lilipofanyika mwili, ndiposa Neno likaonekana.

<sup>254</sup> Na kwa sadaka ya kifo Chake hapo Kalvari, na kufufuka Kwake, aliliweka Kanisa Lake katika milki hiyo, kwamba Mungu yeye yule asiyeonekana angeweza kuja ndani ya mtu na kulifanya Neno lionekane. Loo, jamani! La—laiti kanisa langu lingeweza kupata hilo. Kama mngeweza kuona, marafiki, Mungu asiyeonekana akifanywa aonekane!

Sasa sikilizeni. Hebu na tulichunguze tena sasa.

<sup>255</sup> Mara nyingi nimetaka kuingia kanisani, nimetamani kuliona, nadhani, ambapo ningeweza kuingia kwenye mlango wa nyuma, mlango wa mbele, po pote pale, nitazame kusanyiko na kuona kanisa kamilifu, lote katika utaratibu. Dhambi isingeweza kukaa mle; la, Roho angeitamka, unaona. Isingaliweza kukaa kamwe. Kama Anania na Safira, hu—hungeweza kulitenda kabisa. Hakutakuwa na dhambi katika hilo, kundi hilo. La, bwana. Unaona, Roho upesi analinena *hivyo*. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara nne—Mh.] Haiduru ilikuwa nini, ni ndogo vipi, lingetendeka. Nione wanawake na mwanamume wameketi pale chini ya Uweza wa Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu akitenda kazi kikamilifu, akiongoza hili. Mtu fulani ametenda jambo lisilo sahihi katika kusanyiko, isingewezekana, wangeweza. . . Wasingeweza, inge. . . Wanakuja upesi, na kuliungama kabla Roho hajalishika, kuliungama kabla hawajakuja kulisema, sababu wanajua litatajwa wakati uo huo. Hilo ni kweli. Hilo ni Kanisa la Mungu aliye hai. Jinsi maskini moyo wangu mzee, sasa unazeeka, jinsi nilivyotamani kusimama na kuona kanisa kama hilo. Ningali naweza, hata sasa. Natumaini kuliona. Kazi kamilifu za Mungu, bila dhambi, sasa, ambalo lingeweza kufahamu.

<sup>256</sup> Naam hapa panasimama kundi la watu ili waombewe. Sasa tunatambua, kama Andiko hili ni kweli. . . Na Mungu wa Mbinguni, Ambaye angeweza kuumba kindi, angeweza kuumba kondoo dume, angeweza kusimamisha jua siku nzima, masaa ishirini na manne, ambaye angeweza kuzuia moto usiunguze watu katika tanuru kwa masaa matatu, Yeye aliyefumba vinywa vya simba, ambaye angeweza kufufua wafu, angeweza kutembea juu ya maji, angeweza kuchukua biskuti na kuwalisha elfu tano, huyo ni Mungu. Hilo ni Neno lililofanyika mwili katika wanadamu. Sasa kila mtu anaelewa hilo? Sasa Mungu yuyu huyu aliahidi kwamba katika siku za mwisho mambo haya yangelitendeka tena, bali Yeye hawezi kulitenda mpaka kuwe na mtu fulani ambaye Yeye anaweza kutenda kazi naye na kutenda kazi kwake. Unaona nimaanishalo? Sasa hebu na tuamini hilo, kabisa kabisa, kwa mioyo yetu yote, kwamba itakuwa hivyo.

<sup>257</sup> Sasa hapa panasimama kundi la watu, wengi wao nawajua. Nafikiri. . . Si—si—sidhani, mwanamke huyu wa kwanza hapa mbele, msichana huyu, sidhani ninamjua. Namjua Ndugu Way; na dada yule, yule mwingine pale, Ndugu Roberson. . . au mke wa Borders. Ila simjui mtu anayefuata. Sina budi

kumjua mwanamke anayefuata; sijui, sidhani ninamjua. Ndiyo, ninamjua. Na anayefuatia, yule mwanamume anayesimama pale, kama sijakosea, huyo ni mwana wa Ndugu Daulton. Na, kwenye ile safu pale, karibu namjua kila mtu aliyepo hapo.

<sup>258</sup> Sina habari ni nani. . . ni akina nani, kule wanakotoka. Bali sasa, wanachohitaji sasa ni maombi. Baadhi yao, bila shaka, wako mbali, hawawezi kupata sawasawa ni kitu gani.

<sup>259</sup> Sasa tafadhali kila mmoja wenu aangalie upande huu kwa dakika moja, kila mmoja wenu kwenye mstari wa maombi. Kama ningeweza kukusaidia, ningefanya hivyo. Unaona? Nami nipo hapa kuwasaidia. Bali njia pekee nitawahi kuweza kulitenda, kurejesha ambacho Shetani amewatenda, ni ninyi mnamini mimi. Kama tu mtaniamini mimi, kwa mioyo yenu yote, litatendeka.

<sup>260</sup> Sasa ilikuwa ni desturi, katika huduma yangu, ingesababisha maono. Maono yangetokea, nami niliweza kuwaambia watu kilichowaleta. Na, ninyi, wangapi wameona hilo likitendeka? Loo, ninyi nyote, unaona. Hilo ni kweli. Ndiyo, bado naweza kulitenda. Loo, bado laweza kutendwa. Hakika. Ndiyo. Hiyo ni kweli.

<sup>261</sup> Bali tunakuja kwenye kitu kikubwa kuliko hicho sasa. Ndiyo. Tunapanda juu ya hilo. Unaona, tunakuja kwenye hilo Neno lililonenwa. Na itambidi Shetani kutii; litamfunga katika fundo. Kama nikiweza tu kuwafanya ninyi mliamini! Msilitilie shaka.

<sup>262</sup> Hapa, kama mnataka kujua iwapo ninawaambia kweli, kama Roho Mtakatifu yuko hapa. Najua ambalo, msichana yule, jambo linalomtatiza msichana yule. Simjui, bali najua ana shida gani. Unaona? Ndiyo. Hilo ni sahihi kabisa. Na yeye ananipiga tu vita sana awezavyo, bali itambidi ajisalishe. Ninyi aminini tu hilo. Usilitilie shaka, dada. A-haa. Ndiyo, usilishuku. Ni sawa tu, dada. Wewe, utakuwa mzima. Itakuwa sawa. Unaona?

<sup>263</sup> Hapa pana mtu mweusi anayeniangalia, amesimama pale kwenye mstari. Mimi sikujui, bali Mungu anakujua. Iwapo ningekwambia matatizo yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Utaniamini? Hupo hapa kwa ajili yako binafsi. Huyo mtoto huko hospitalini atakuwa mzima iwapo utaamini. Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Basi nenda zako, rudi ukaketi. Ninatamka Nguvu za Mungu juu ya mtoto huyo; ibilisi amwachilie.

<sup>264</sup> Daulton mdogo akiniangalia, upo hapa kwa ajili ya mtoto yule mchanga. Mtoto yule mchanga ana matatizo ya kitovu chake. Sivyo? Rudi ukaketi, nawe liamini, naye atapona tu.

<sup>265</sup> Ninamtazama mwanamke mwingine ameketi pale, ni Bi. Stricker. Bibi Stricker, sijazungumza nawe kwa miezi. Sina habari upo hapa kwa ajili gani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia tatizo lako? Je, litawafanya ninyi nyote muamini?

Upo hapa kwa ajili ya mtoto yule mdogo aliye na tatizo la mguu wake. Pia, unaomba kwa ajili ya rafiki aliyeko Afrika. Hilo ni kweli kabisa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa iwapo hilo ni kweli, Bibi Stricker, inua mkono wako juu. Unaona?

<sup>266</sup> Yeye yupo hapa; unaona. Ila hiyo-hiyo huduma itakuwepo sikuzote, bali hapa yaja nyingine. Aminini sasa! Msishuku. Hata mmoja wenu asishuku. Ninapoweka mikono yangu juu yako, na kuomba hili lifanyike, litafanyika. Jambo pekee tu, ni kama tu kuchukua Neno la Mungu. Jambo pekee, kama huamini Hilo, halitafanyika. Kama unaamini Hilo, lazima litukie. Kwa kuwa, kitu fulani kilitukia usiku wa juzijuzi kule, nami najua Mungu yeye yule ambaye aliweza kuumba angeweza kulitenda. Sawa.

<sup>267</sup> Nataka watu wote wainamishe vichwa vyao. Kila mmoja awe katika maombi. [Ndugu Branham anaondoka mimbarani, kuwaombea wale walio katika mstari wa maombi—Mh.]

Wewe ibilisi uliyemfunga Sharon, huyu msichana mdogo mzuri!

<sup>268</sup> Yule, Mungu, Yeye ambaye alinipa ono usiku wa juzijuzi la ibilisi akifungwa, na akasema, “Katika uaminifu, unaweza kumfunga.” Na kwa uaminifu wa moyo wangu kwa mtoto huyu. Nimekuja, Bwana, kuomba rehema na upendeleo Wako, kwa ajili yake.

<sup>269</sup> Shetani, ninakufunga. Katika Jina la Yesu Kristo, muache mtoto huyu. Ili kwamba akili zake na fahamu zake zimrudie, kama kawaida. Hivyo Neno limenenwa, hivyo litatendeka katika Jina la Yesu Kristo.

<sup>270</sup> Bwana Mungu, kwa ajili ya Ndugu yangu Way, jalia kwamba Uweza wa Yesu Kristo uzifunge nguvu za ibilisi anayemfunga ndugu yangu. Kisha muweke huru, katika Jina la Yesu Kristo.

<sup>271</sup> Mungu, maskini mwanamke huyu atakuwa kama yule wa kwanza hapa, katika majuma machache, iwapo hakuna jambo litakalofanyika kwake. Ni mke wa ndugu yangu, Ndugu Roy. Bwana Yesu, nipe nguvu sasa. Wewe Ambaye ulitoa ono lile, Wewe hujashindwa, Hilo halijashindwa kamwe.

<sup>272</sup> Ewe roho wa ibilisi, ambaye umemfunga dada yangu, ninakufunga. Katika Jina la Yesu Kristo, muache. Limekwisha nenwa, hivyo na litendeke . . . ? . . . sawa.

<sup>273</sup> Katika Jina la Bwana Yesu, mtoe dada yetu katika matatizo yake. Katika Jina la Kristo Ambaye aliahidi, na akatoa ahadi, “Kama ukiuambia mlima huu.” Jalia na litendeke, Bwana.

<sup>274</sup> Juu ya mwanamke huyu anayehisi upako wa Roho Mtakatifu humu chumbani. Ninaweka mikono yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya Roho yake. Katika . . . Hebu na litendeke, kwani limekwisha nenwa. Amina.

<sup>275</sup> Juu ya msichana huyu mdogo, JoAnn, nikiweka katika nia yangu mfano wa msichana mdogo wa Kikristo. Ninamfungua

asubuhi hii, kutoka kwenye jambo hili baya. Katika Jina la Yesu Kristo, ombi lake na lijaliwe.

276 Bwana Mungu, juu ya huyu mwenzi mpenzi wa ndugu yangu mpenzi, Dada Thorns. Hebu nimkaribie yule mwovu ambaye angemfunga na afungwe. Katika Jina la Yesu Kristo, na awe huru.

277 Juu ya dada yangu, naweka mikono yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, uweza wa adui na ufungwe. Kwamba dada yetu, atakuwa huru tangu leo.

278 Juu ya ndugu yangu, naweka mikono yangu, sawasawa na Neno la Mungu. Pepo ambaye angemdhuru na kumzuia, na amtoke. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

279 Kwa ajili ya ombi la dada yangu, ninaomba kwamba utalijibu, Bwana. Ninapoweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, hebu na litendeke. Amina.

280 Kwa ajili ya dada yangu, Baba, ninapoweka mikono yangu juu yake. Katika Jina la Yesu Kristo, ombi lake na lijibiwe. Amina.

281 Kwa imani nyofu, Bwana, ingawa ni nyofu—ni kitendawili, kuweka mikono yangu juu ya hawa ndugu. Katika Jina la Bwana Yesu, hebu ombi lake na lijibiwe.

282 Juu ya Dada yangu Way, ambaye amewarehemu wale waliohitaji rehema. Na imeandikwa, “Hao watapata rehema.” Jalia kwamba rehema ambazo anaomba asubuhi hii, akirimiwe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

283 Bwana, maskini, mama huyu aliyevunjika moyo, unajua ombi lake, Ee Mungu wa Milele, na ajibiwe leo. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

284 Basi Baba Mungu, kwa dada yangu, naiweka mikono yangu juu yake, kama nilivyoagizwa na Roho Mtakatifu pamoja na lile ono usiku wa juzijuzi. Ombi lake na lijibiwe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

285 Baba wa Mbinguni, wakati dada huyu anakuja juu hapa kuchukua mahali pake, apate kuwekewa mikono. Jibu ombi lake, Ee Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, na lifanyike.

286 Baba wa Mbinguni, ninapoushika huu, mkono wa dada yangu, Uweza wa Yesu Kristo na ujibu ombi lake. Amina.

287 Bwana Yesu, ninapoushika mkono wa huyu dada, na ile leso...?...ombi lake na lijibiwe. Katika Jina la Yesu Kristo, lijalie. Amina.

288 Baba Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, ombi la dada yetu na lijibiwe. Kile anachoomba, na akipokee. Katika Jina la Yesu Kristo.

Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu;  
Hebu amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu.

<sup>289</sup> Sasa kabla tu ya kutawanyika, hebu nichukue fursa moja au mbili ya muda wenu. Kitendawili, Mungu ametenda hicho. Mbele zetu hasa, kitendawili kimekwisha tendeka. Kwani nilipoanza tu kwenda kwenye mstari ule wa maombi, Kitu fulani kiliniinua tu juu, sawasawa tu kabisa na Yeye alivyosema ingetendeka. Unaona, kitendawili! Unaona?

<sup>290</sup> Na hapo Roho alipokuwa juu yangu namna hiyo, niliweza kuangalia chini kwenye ule mstari na kuona mambo yale ambayo watu wale walikuwa wanahitaji, unaona. Kwa hiyo, kama watatu au wanne kati yao, au kitu fulani, kusudi iwe uthibitisho, ushahidi, kwamba Mungu kamwe haondoi kipawa ambacho ni kipawa cha kweli. Yeye huongezea tu kwenye hicho, na kinaendelea tu kuwa bora zaidi.

<sup>291</sup> Sasa ninaamini, kwa moyo wangu wote, kwamba mmeponywa. Amina. Ninaliamini kwa yote yaliyomo ndani yangu. Na—naamini hilo.

<sup>292</sup> Naam, Yesu aliwakaribisha kuja kwenye wokovu. Kama ungekuja, ungeupata Huo, sababu Yeye aliahidi jambo hilo. Yeye aliahidi hilo, basi sasa tusilitilie shaka. Bali na tuliamini kwa moyo wetu wote. Naam, msilipinge, jueni tu kwamba linapaswa kutendeka. Lazima litendeke. Yesu alisema, “Nena Neno hili. Usilishuku.” Unaona? Na Yeye ndiye Huyu hasa.

<sup>293</sup> Basi hayo maono, kadiri nijuavyo, kwa moyo wangu wote, hata wakati mmoja hayakushindwa, hata wakati mmoja. Na Yeye alisema, usiku wa juzijuzi, na (wale) niliowaambia lile ono, mbele za Mungu ninayesimama mbele Zake, hilo ni kweli, unaona. Yeye aliona nyoka yule akifungwa. Akasema, “Itakubidi uwe mwaminifu zaidi.”

<sup>294</sup> Hicho ndicho ninachopigania, ni uaminifu zaidi. Na kila mmoja anayekuwa humu asubuhi hii, nilijaribu kuwaza, “Je! kama yule angekuwa ni mama yangu, hao wanawake, kama huyo alikuwa dada yangu akitiye nyuma kule, kama huyo angekuwa mke wangu ameketi nyuma kule, au mmoja wa watoto wangu ameketi nyuma kule, vipi kama ingekuwa wao?” Nikijaribu kujiweka mwenyewe mahali pao, kuwa mwaminifu. Na kama uliangalia, kile hasa . . .

<sup>295</sup> Naam, inanikumbusha jambo fulani. Hivi majuzi, nilipokuwa California, na kusimama kwenye kiamshakinywa cha Wafanyi Biashara. Nadhani ninalo hapa. Nina uhakika kabisa. Nilikuwa ninaliangalia muda mchache uliopita, unabii ambao ulitolewa. Huu papa hapa. Huu ulitolewa, baada ya kusimama na kuhubiri mahubiri makali. Na watu wapo hapa asubuhi hii; Ndugu Roy Borders, akiwa mmoja, aliyekuwepo,

ninaamini, po pote alipo Roy, alipokuwepo, ndiyo, ameketi hapa; alikuwepo pale wakati hili lilipokuwa linatukia, na wengine wengi ambao walikuwepo pale. Wakati, mvulana ambaye alikuwa Mbatisti, ilikuwa mpwawe Jane Russell, mchezaji mashuhuri wa sinema; ye yote anayetaka kuja kwenye hicho kiamshakinywa anaweza kuja. Nami nilipomaliza kuzungumza, yule mvulana alikuja kunikumbatia, akasema . . .

<sup>296</sup> Nilipoondoka kwenye jukwaa moja, nikishuka hadi kwenye jingine, ili kulizungumzia kusanyiko, ambapo, mamia kadhaa walikuwepo. Nami nilikuwa nikizungumza kwenye—matangazo ambayo yalisikika nchini kote mnamo saa tatu usiku uliofuata. Ulikuwa unanaswa kwenye kanda wakati huo. Na wakati hii . . . Niliposhuka kwenye jukwaa hili jingine, kuzungumza wakati mwingine, kwa watu hawa *hapa*. Na moja ya madhehebu makubwa yalikuwa na mmoja wa viongozi wao, amesimama pale, naye alikuwa anauchukia ule Ujumbe, unaona, kwa kusema . . .

<sup>297</sup> Nilikuwa ninazungumza kuhusu nilipokuwa huko Phoenix, siku chache hapo kabla, na jinsi niliona matunda mengi tofauti yakiota kwenye mti mmoja. Niliangalia katika mchungwa, mlikuwemo na balungi, ndimu, nami naamini chenza, na kangaja, na namna zote za vitu hivyo zikimea, sababu ni mti jamii ya mibalungi. Bali nikasema, “Kila mwaka huchanua na kuzaa matunda mapya. Lakini kuna tu yale matawi ya asili; unapochanua, wakati mti halisi unapochanua tawi lingine, linazaa aina ile ile ya tunda ambalo limo katika lile shina. Bali hii miti mingine huzaa matunda yao, ingawa inaishi kwa u—uhai wa mti huu.” Nikasema, “Hilo ni kama madhehebu yakiwekwa kwenye ule Mzabibu. Yesu alisema, ‘Mimi Ndimi mzabibu.’ Na kila wakati ambapo huo Mzabibu unatoa tawi, litakuwa tu kama huo Mzabibu. Unaona, litazaa tunda lile lile.”

<sup>298</sup> Naam, huyu mhudumu maarufu wa madhehebu yaliyo makubwa sana ya Kipentekoste tuliyokuwa nayo, alikuwa amesimama pale, naye aliuchukia Huo, unaona, akasema kwamba sikulimaanisha namna hiyo.

<sup>299</sup> Bali nilirudi na kusema, “Ninamaanisha hilo namna hiyo, unaona. Nilisema sawa kabisa! Sighairi kitu.”

<sup>300</sup> Juzijuzi nilipozungumza kuhusu zile madhabahu, bila kujua, kamwe sijaona kwenye historia. Sijasema neno lo lote bado, jukwaani, chini ya upako, ambalo niliwahi kughairi. Sasa waweza kurejea kwa huo, *Uzao Wa Nyoka*, au wo wote unaotaka, Ujumbe wo wote ule, au, *Yule Kahaba Mkuu*, ambapo ndipo penye upinzani mwingi sana. Njoo tu, kwa nini usije kwangu na Maandiko, na jambo hilo, unaona, uone kama ni sahihi.

<sup>301</sup> Mtu huyu alipanda akaja pale, akanikumbatia, na alitaka kusema . . . Akasema, “Ndugu Branham, sitaki kukufuru, bali huo ungefanyiza sura ya 23 ya Ufunuo. Wajua, Kitabu kingine

kiongezwe. Bila shaka,” yeye alisema, “hilo lisingekuwa sahihi, bila shaka, hatupaswi kuongezea kitu cho chote Kwake.” Na mara tu alipoanza kusema hilo, akaanza kunena kwa lugha. Na yule mvulana hakujua kunena kwa lugha ni nini.

<sup>302</sup> Na mara tu aliponena; papo hapo mbele yangu palikuwa na mwanamke Mfaransa, toka Louisiana, akasema, “Hilo halihitaji tafsiri yo yote. Hicho kilikuwa Kifaransa halisi.”

Kisha mtu mwingine upande huu akasimama akasema, “Hilo ni sawa.”

<sup>303</sup> Na huko nyuma kabisa alikuwepo mkalimani wa Umoja wa Mataifa, akatoa jina lake, hajawahi kuwepo pale hapo kabla. Akasema, “Ni sawa. Hilo ni sawa.”

<sup>304</sup> Na haya hapa ndiyo waliyokusanya pamoja. Na kila mmoja wao alikuwa na jambo lile lile walipokutana, kila mmoja wao akitoa tafsiri, sawasawa kabisa.

<sup>305</sup> Na huyu mwanamume Mfaransa, wa pili aliyekuwa upande huu, aliliandika, kwa sababu alikuwa akiandika taarifa za mkutano ule. Haya hapa ndiyo aliyoandika. “Mimi, Victor Le Dioux, mimi ni Mfaransa, Mfaransa halisi, Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Ninaishi huko 809 North Kings Road, Los Angeles 46. Ninashiriki katika Bethel Temple, Arnie Vick ndiye mchungaji wetu,” mhudumu wa Kipentekoste, kanisa lililo kubwa sana la Kipentekoste katika Los Angeles. “Tafsiri ya unabii juu ya Ndugu Branham, uliotolewa na Danny Henry, katika Kifaransa, Februari 11, 1961, kwenye kiamshakinywa cha Wafanya Biashara wa Injili Yote; tafsiri ya kweli ya unabii huo.” Wote watatu wao walisema hii ndiyo.

*Kwa sababu wewe umechagua ile njia nyembamba . . .*

<sup>306</sup> Mnaona, ni kinyume tu, itanibidi niipitie peke yako, unaona. Naweza kuelewa hilo. Ilimbidi Musa ajiamulie, pia. Unaona? Haikumlazimu kufanya jambo hilo, bali alilifanya. Unaona? “Njia iliyo ngumu zaidi; wewe . . .” Mnaona?

*Kwa sababu wewe umechagua ile njia nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi; wewe umejanya . . . wewe umeenenda kwa hiari yako.*

<sup>307</sup> Kwa maneno mengine, haikunilazimu kufanya hivyo. Naweza kujiunga nao, niandamane nao kama nikitaka. Bali nilidumu na . . . nataka kudumu na Neno.

*Wewe umejanya uamuzi ulio sahihi na sawa kabisa, na ndiyo NJIA YANGU.*

<sup>308</sup> Kama utachunguza, limewekewa vituo na kupigiwa mstari. Kama ukichunguza, yameandikwa katika Kifaransa, haya; yamenenwa katika Kifaransa, kiarifa kabla ya kisifa, unaona.

*Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa ya Mbingu inakungojea.*

309 Sasa, hilo ndilo lililoni shangaza. Nitakapokufa, je, itawakuwa wakati huo? Basi nikawaza, “Mbinguni hakukugawanywa visehemu mbalimbali kwa ajili yetu huko juu; Mbinguni ni Ufalme wa Mbinguni ambao umo ndani yetu, mtu anaungojea.” Unaona? Sasa angalia.

*Ni uamuzi wenye fahari vipi uliofanya!*

*Jambo hili lenyewe ndilo litakalotoa na kusababisha ule ushindi mkuu katika upendo wa Kiungu.*

310 Unaona, sisi tungenesema, “Katika ushindi mkuu katika upendo wa Kiungu,” bali katika Kifaransa ingekuwa “Wa Kiungu upendo.” Kama Kijerumani tu au nyingine yo yote, unaona, wanaweka ile . . . huweka kiarifa mbele ya kisifa.

311 Sasa unaona kushuka kwenda Yordani kulimaanisha nini? Tumefikia hapa sasa. Hebu na tuvuke sasa. Tuache kucheza. Na tuvuke ng’ambo ya pili sasa, sababu yote ni mali yetu. Yote ni yetu. Hayo maono hayajashindwa kutimia. Hayawezi kushindwa, kwa sababu yanatoka kwa Mungu. Ninaamini hilo kwa yote yaliyo ndani yangu. Sisi si vibaraka ambao watarudi mbio nyikani. Tutavuka Yordani, ule utenganisho. Mungu, tuvunjie zile Muhuri ambazo ziko nyuma ya kile Kitabu! Tujalie tuingie katika sehemu hii kuu sasa, kwani Yoshua aliwagawia watu urithi wao ambao Mungu aliwaachia.

312 Na kama ulichunguza, hao mama wa Kiebrania walipokuwa katika utungu wa kuzaa na wakawazaa wale wazee. Nitalifikia hilo, mojawapo ya siku hizi, Bwana akipenda. Na wakawazaa wale wazee, alipotamka majina yao, katika utungu wa kuzaa, yeye pia aliwaweka mahali pao halisi katika ufalme. Loo, jamani!

313 Uvuvio ni—ni kitendawili. Unaona, hu—huwezi tu kulishika. Bali limevuviwa, na Mungu huliweka moja kwa moja katika sehemu yake, kwenye—kwenye saa usiyodhania.

314 Sasa, kama hakuna theluji sana, na tukaweza, Bwana akipenda, Jumapili ijayo nataka kuzungumzia juu ya somo la *Ukristo Dhidi ya Ibada Ya Kipagani*. Na kama unaweza, njoo na karatasi yako, lo lote unalotaka, kwa ajili ya huo Ujumbe. Jumbe zitaendelea tena usiku wa leo, ndugu. . . baadhi ya hawa ndugu hapa, nadhani, watahubiri. Nilikuwa nibaki, bali najua wengi wa watu watabaki, na imebashiriwa kutakuwa na theluji tena alasiri hii, itakayofunika barabara kabisa, kuanzia Georgia na sehemu mbalimbali. Kwa hiyo mimi. . . Bwana akipenda, Jumapili ijayo, nilikuwa naenda kuzungumzia Ujumbe ule ule usiku wa leo, bali nitauahirisha hadi Jumapili na baadaye. Mungu awe pamoja nanyi.

<sup>315</sup> Naamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliye hai, aliyezaliwa na bikira, akachukuliwa mimba, Mungu katika tumbo la uzazi, maskani ambamo Yeye angekaa. Ninaamini kwamba, katika Kristo, Yeye ni Mungu aliyefanyika mtu. Yeye ni Mungu aliyefanyika mwili. Wakati Baba Mungu alipokuja ndani ya Yesu Kristo, Yeye alikuwa utimilifu wote wa Uungu kwa jinsi ya mwili, ndani Yake unakaa utimilifu wote. Mungu Baba alinena Maneno yale. Yesu alisema, “Si Mimi ninayezungumza, bali Baba yangu akaaye ndani Yangu. Yeye ndiye anayezungumza.” Kwa hiyo juu ya msingi huo, Yeye akifanyika mwili kusudi Yeye aweze kufa; Mungu akilipa ile adhabu kwa ajili ya wanadamu, kukomboa na kuinua, na—na kuja, kuleta pamoja mambo ambayo umbaji Wake Mwenyewe umepoteza katika lile anguko, Yeye aliwakomboa kwa uhai Wake Mwenyewe.

<sup>316</sup> Basi, katika kuwakomboa watu hawa, kusudi Injili Yake iendelee, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, pia. Nyingi zaidi ya hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba. Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona Mimi; kwa kuwa Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu.” Saa tumefikia mwisho wa wakati. Kristo amerudi katika hali Yake ya Roho Mtakatifu, katika utimilifu wa Uweza Wake, katika Kanisa, kujidhihirisha Mwenyewe. Ni rahisi. Ni watu wa kawaida.

<sup>317</sup> Kama kungekuwa na mtu fulani hapa ambaye ana bahati ya kutosha kuwa na elimu nzuri, na labda aende kwenye kanisa kubwa, usiruhusu urahisi wa tabaka hii ya watu maskini uwakwaze. Unaona? Si, si hilo. “Watu wa kawaida walimsikiliza Yeye kwa furaha.” Unaona, ni watu wa kawaida.

<sup>318</sup> Sasa kuna, kuna tabaka za watu. Kuna wengine ambao kweli hawajali, huishi maisha ya namna yo yote, wako huko mitaani, na kadhalika. Hao sio wale waliomsikiliza Yeye. Na hao wa tabaka ya juu, hao sio waliomsikiza. Ilikuwa ile ta—tabaka ya kati, watu wa kawaida, wale ambao ni maskini ambao hata hivyo wanataka kuishi maisha masafi na mastahifu, nao wanataka kumwishia Mungu, hao ndio wanaomsikia Yeye.

<sup>319</sup> Hivyo, hebu mimi na wewe tuwe watu ambao watakaomsikia Yeye katika zamani hizi, kwani kwa kweli ninaamini kwamba moja ya mambo makubwa sana yaliyopata kutukia ulimwenguni yanatukia sasa. Amina. Mungu awabariki.

Sasa nitairudisha ibada kwa Ndugu Neville.



*KITENDAWILI* SWA61-1210

(Paradox)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi Desemba 10, 1961, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)